# Language: Swahili

## Book: Hebrews

---

## Hebrews

### Chapter 1

1 Nyakati zilizopita Mungu alizungumza na mababu zetu kupitia manabii mara nyingi na kwa njia nyingi.
2 Lakini katika siku hizi tulizonazo, Mungu ameongea nasi kupitia Mwana, ambaye alimweka kuwa mrithi
wa vitu vyote, na ambaye kupitia yeye pia aliumba ulimwengu. 3 Mwanawe ni nuru ya utukufu wake, tabia
pekee ya asili yake, na anayeendeleza vitu vyote kwa neno la nguvu zake. Baada ya kukamilisha utakaso
wa dhambi, aliketi chini mkono wa kulia wa enzi huko juu. 4 Amekuwa bora kuliko malaika, kama vile jina
alilolirithi lilivyo bora zaidi kuliko jina lao. 5 Kwa maana ni kwa malaika gani aliwahi kusema, "Wewe ni
mwanangu, leo nimekuwa baba yako?" Na tena, "Nitakuwa baba kwake, naye atakuwa mwana kwangu?"
6 Tena, wakati Mungu alipomleta mzaliwa wa kwanza ulimwenguni, husema, "Malaika wote wa Mungu
lazima wamwabudu." 7 Kuhusu malaika asema, "Yeye ambaye hufanya malaika zake kuwa roho, na
watumishi wake kuwa ndimi za moto." 8 Lakini kuhusu Mwana husema, "Kiti chako cha enzi, Mungu, ni
cha milele na milele. Fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki. 9 Umependa haki na kuchukia uvunjaji wa
sheria, kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekupaka mafuta ya furaha kuliko wenzako." 10 Hapo mwanzo,
Bwana, uliweka msingi wa dunia. Mbingu ni kazi za mikono yako. 11 Zitatoweka, lakini wewe utaendelea.
Zote zitachakaa kama vazi. 12 Utazikunjakunja kama koti, nazo zitabadilika kama vazi. Lakini wewe ni
yuleyule, na miaka yako haitakoma." 13 Lakini ni kwa malaika yupi Mungu alisema wakati wowote, "Keti
mkono wangu wa kulia mpaka nitakapowafanya adui zako kuwa kiti cha miguu yako"? 14 Je, malaika wote
siyo roho zilizotumwa kuwahudumia na kuwatunza wale watakaourithi wokovu?

---

### Waebrania 01 Maelezo kwa jumla

#### Muundo na Mpangilio

Sura hii inaonyesha jinsi Yesu ni muhimu kwa sisi kuliko malaika.

Watafsiri wengine wametenga kila mshororo wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 1:5, 7-13, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

#### "Mababu wetu"

Mwandishi aliandikia barua hii Wakristo waliokuwa wamekua kama Wayahudi.Hii ndiyo maana barua hii inaitwa "Waebrania".

#### Mifano muhimu ya hotuba

#### Maswali ya hadithi

Mwandishi anatumia maswali ya hadithi kama njia ya kuthibitsha kwamba Yesu ni bora kuliko malaika. Yeye pamoja na wasomaji wake wanafahamu majibu ya maswali na mwandishi anajua kwamba wakati wasomaji wanafikiria juu ya majibu ya maswali, watakuja kufahamu kwamba Mwana wa Mungu ni muhimu kuliko malaika wowote.

#### Ushairi

Walimu Wayahudi sawa na manabii wa Agano la kale, waliyaweka masomo yao mengi ya muhimu kwa ushairi ili wasikilizaji waelewe na kuyakumbuka.

---

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

### Hebrews 1:1

**Sentensi Unganishi:**
Hii inaweka msingi wa kitabu chote: Ukuu wa Mwana- Mwana ni mkuu kuliko wote. Kitabu kinaanza na msisitizo kwamba Mwana ni mkuu kuliko manabii na malaika.

**Maelezo ya Jumla:**
Ingawa haijaelezwa mwanzoni mwa kitabu, barua hii iliandikwa kwa Waebrania Wakati (Wayahudi) ambao kimsingi walikuwa wanaelewa maelekezo mengi ya Agano la Kale.

**Kupitia Mwana**
''Mwana" ni cheo muhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu.

**Mungu kuwa mrithi wa vitu vyote**
Mwandishi anamwelezea kana kwamba Mwana atarithi utajiri na mali kutoka kwa Baba. AT: " kumilili vitu vyote"

**Mungu aliuumba ulimwengu kupitia yeye**
"Ni kupitia yeye pia Mungu aliviumba vitu vyote.

**Mwana**
Hiki ni cheo muhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu.

**mng'ao wa utukufu wa Mungu**
"mwanga wa utukufu wake.'Utukufu wa Mungu una muunganiko wa mng'ao sana. Mwandishi anasema Mwana anabeba mng'ao huo na anamwakilisha Mungu kwa ukamilifu.

**tabia sawa ya asili yake**
"sura ya Uungu wa mungu." Hii ina maana sawa na "mng'ao wa utukufu wa Mungu" Mwana anabeba tabia na asili ya Mungu na anawakilisha uungu wote wa Mungu. inaweza kusemwa katika

**neno la nguvu zake**
"neno lake la nguv." Hapa "neno" linamaanisha ujumbe au amri. AT: "amri yake ya nguvu"

**Baada ya kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi**
Jina dhaniwa"takasa" linaweza kuelezea kama kitenzi: "kufanya safi." AT: "Baada ya kumaliza kutufanya kuwa safi' au baada ya kumaliza kututakasa kutoka katika dhambi zetu"

**amefanya utakaso kwa ajili yetu**
Mwandishi anaongea juu ya msamaha wa dhambi kana kwamba ulikuwa unamfanya mtu kuwa safi. AT: amefanya uwezekano kwa ajili ya Mungu kusamehe dhambi"

**aliketi katika mkono wake wa kuume wa mwenye enzi"**
Hapa "mkono wa kulia" linamaanisha sehemu ya utukufu.AT: "aliketi katika sehemu ya utukufu karibu na kwenye enzi"

**Mwenye enzi aketiye juu**
"Hapa "enzi" linamaanisha Mungu. AT: "Mungu mwenye enzi

### Hebrews 1:4

**maelezo ya Jumla:**
Hii ni nukuu ya kinabii (Wewe mwanangu) inatoka katika Zaburi. Nabii Samweli aliandika unabii wa pili (nitakuwa baba kwake). Maneno yote ambaye yanamaanisha Yesu. Neno "Wewe" linamaana ya Yesu, na neno "Mimi" linamaanisha Mungu Baba.

**Amekuwa**
''Mwana amefanyika"

**Kama jina alilorithi ni bora zaidi ya majina yao Kwa malaika gani aliwahi kusema ...baba"?**
Mwanaidishi anaongea katika swala la kupokea heshima na mamlaka kana kwamba alikuwa akirithi utajiri na mali kutoka kw baba yake.AT: "amepokea."

**Ni malaika wapi Mungu alimewahi kuwambia "Wewe ni mwanangu... mwana kwangu"?**
Swali linasistiza kuwa Mungu hamwita malaika yeyote mwana wake. AT: " kwa sababu Mungu hajawahi kumwabia malaika yeyote 'Wewe ni mwana wangu... mwana kwangu."

**Na tena...kwangu**
"Na tena, hakuwahi kusema kwa malaika yeyote, '...kwangu'?"

**Wewe ni mwanangu...nimekuwa baba yako...nitakuwa baba kwake...atakuwa mwana kwangu**
Uhusiano maalumu Mungu Baba alionao na Mungu Mwana umeelezwa katika Agno la Kale mamia ya miaka kabla ya Yesu kuzaliwa.

**Wewe ni mwanangu... nimekuwa baba yako**
maneno haya kimsingi yanamaanisha kitu kimoja.

### Hebrews 1:6

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu ya kwanza katika sehemu hii (Malaika wote wa Mungu...) inatoka katika moja ya kitabu alivyoandika Musa. Na nukuu ya pili (Yeye afanyaye ...) inatoka katika kitabu cha Zaburi.

**Mzaliwa wa kwanza**
Hii inamanisha Yesu.Mwandishi anamwelezea Yesu kama "mzaliwa wa kwanza" kusisitiza umuhimu na mamlaka juu ya mtu yeyote. Haina maana ya kuwa kulikuwa na wakati fulani ambao Yesu hakuwepo au kwamba Mungu alikuwa na wana kama Yesu. AT: "Mwana wake mheshimiwa, Mwana wake wa pekee.

**akasema**
"Mungu anasema"

**Yeye awafanyaye malaika wake roho, na watumishi wake miali ya moto**
Maana inayowezekana: 1) "Mungu amewafanya malaika wae kuwa roho zinazomtumikia kwa nguvu kama miali ya moto." (UDB) au 2)Mungu hufanya upepo na miali ya moto kuwa "watumwa" na watumishi wake. Katika lugha za asili neno "malaika" ni sawa na neno "mtumishi," na neno "roho" ni sawa na "upepo." Kwa maana yoyote ile ujumbe kusudiwa ni kwamba malaika wanamtumika Mwana kwa kuwa ni mkuu,

## Hebrews 1:8

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii ya andiko inatoka katika kitabu cha Zaburi

**Kuhusu Mwana anasema,**
"Lakini Mungu asema hivi kuhusu Mwana"

**Mwana**
Hiki ni cheo muhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu.

**Kiti chako cha enzi, Mungu ni cha milele**
Kiti cha enzi kinawakilisha utawala. AT: " Wewe ni Mungun na utawala wako utadumu milele"

**fimbo yako ya ufalme ni ya haki**
Fimbo yautawala inamaanisha utawala wa Mwana. AT: "Na utatawala juu ya watu katika ufalme wako kwa haki"

**amekupaka mafuta ya furaha zaidi ya wenzako**
Hapa "mafuta ya furaha" inamaanisha furaha aliyokuwa nayo wakati Mungu alipo muheshimu. AT:"amekuheshimu na amekufanya kuwa na furaha zaidi ya yeyote.

## Hebrews 1:10

**Sentensi Unganishi:**
Mwanadishi anaendelea kufanua kwamba Yesu ni mkuu kwa malaika.

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii inatoka katika Zaburi.

**Hapo mwanzo**
"Kabla ya kitu chochote hakijakiwapo"

**uliweka misingi ya nchi**
Mwandishi anaongea Mungu kuumba dunia kana kwamba anajenga juu ya msingi. AT: " uliumba dunia"

**Mbingu ni kazi za mikono yako**
Hapa "mikono" inamaanisha nguvu na matendo ya Mungu.AT: "uliziumba mbingu"

**Zitaharibika**
"Mbingu na nchi zitapotea" au " mbingu na nchi hazitakuwepo tena"

**zitachakaa kama kipande cha nguo**
Mwandishi anaongea juu mbingu na nchi kama ilikuwa ni kipande cha vazi ambayo itazeeka na mwishowe na kutofaa.

**atazianua kama vazi**
Mwandishi anaongea kana kwamba mbingu na na nchi ni nguo au aina nyingine ya vazi.

**Vitabadilishwa kama kipande cha nguo**
Mwandishi anaongea juu ya mbingu na na nchi kana kwamba ni nguo ambazo zinaweza kubadlishwa

**zitabadilishwa**
Hii inaweza kusema katika muundo tendaji. AT: "utazibadilisha"

**Miaka yako haina mwisho**
Vipindi vya nyakati vinatumika kuwakilisha Uwepo wa Mungu wa milele.AT: "maisha yako hayatakuwa na mwisho"

## Hebrews 1:13

**Maelezo ya Jumla**
Nukuu hii inatoka katika Zaburi nyingine.

**Lakini ni malaika gani wakati wowote Mungu amesema...miguu?**
Mwandishi anatumia swali kusisitiza kwamba Mungu hajawahi kumwambia malaika. AT: '"Lakini Mungu hajamwambia malaika yeeyote wakati wowote"'

**Keti mkono wangu wa kulia**
Hapa mkono wa kulia unamaanisha sehemu ya heshima. AT: "Kaa karibu yangu katika sehemu ya heshima"

**Hadi nitakapo waweka maadui wako chini ya miguu yako**
Maadui wa Kristo wanaongelewa kana kwamba watakuwa chombo ambachomfalme anaweka miguu yake, Picha hii inawakilisha kushindwa na aibu kwa maadui wake.

**Sio malaika wote ni roho... wanarithi wokovu**
Mwandishi anatumia hili swali kuwakumbusah wasomaji wake kwamba malaika hawana nguvu kama Kristo, lakini wana jukumu tofauti. AT: "malakia wote ni roho ambazo... hurithi wokovu."

**kwa wale watakaorithi wokovu**
Kupokea kile ambacho Mungu amewaahidi waumini imeongelewa kana kwamba wanarithi utajiri na mali kutoka katika mwana familia. AT: "kwa ajili ya wale wote ambao Mungu atawaokoa"

## Chapter 2

1 Kwa hiyo ni lazima tuweke kipaumbele zaidi kwa yale tuliyosikia, ili kwamba tusije tukatengwa mbali
nayo. 2 Kwa maana ikiwa ujumbe uliozungumzwa na malaika ni halali, na kila kosa na uasi hupokea
adhabu tu, 3 tutapataje kuepuka kama tusipojali wokovu huu mkuu? —wokuvu ambao kwanza
ulitangazwa na Bwana na kuthibitishwa kwetu na wale waliousikia. 4 Mungu pia aliuthibitisha kwa ishara,
maajabu, na kwa matendo makuu mbalimbali, na kwa zawadi za Roho Mtakatifu alizozigawa kulingana na
mapenzi yake mwenyewe. 5 Mungu hakuuweka ulimwengu ujao, ambao tunaongelea habari zake, chini ya
malaika. 6 Badala yake, mtu fulani ameshuhudia mahali fulani akisema, "Mtu ni nani, hata uweze
kumkumbuka? Au mwana wa mtu, hata umtunze? 7 mtu kuwa mdogo kuliko malaika; umemvika taji ya
utukufu na heshima. (Zingatia: Katika nakala halisi za kwanza, mstari huu haupo. "Na umemuweka juu ya
kazi ya mikono yako.) 8 Umeweka kila kitu chini ya miguu yake." Kwa hiyo Mungu ameweka kila kitu chini
ya mtu. Hakuacha kitu chochote ambacho hakiko chini yake. Lakini sasa hivi hatuoni bado kila kitu kikiwa
chini yake. 9 Hata hivyo, tunaona ambaye alikuwa amefanywa kwa muda, chini kuliko malaika—Yesu,
ambaye, kwa sababu ya mateso yake na kifo chake, amevikwa taji ya utukufu na heshima. Hivyo sasa kwa
neema ya Mungu, Yesu ameonja kifo kwa ajili ya kila mtu. 10 Ilikuwa sahihi kwamba Mungu, kwa sababu
kila kitu kipo kwa ajili yake na kupitia yeye, alipaswa kuwaleta watoto wengi katika utukufu, na kwamba
alipaswa kumfanya kiongozi katika wokovu wao kuwa mkamilifu kupitia mateso yake. 11 Kwa maana wote
wawili yule anayeweka wakfu na wale ambao wanawekwa wakfu, wote wanatoka kwenye asili moja,
Mungu. Kwa sababu hii yule anayewaweka wakfu kwa Mungu haoni aibu kuwaita ndugu. 12 Anasema,
"Nitatangaza jina lako kwa ndugu zangu, nitaimba kuhusu wewe kutoka ndani ya kusanyiko." 13 Tena
asema, "Nitaamini katika yeye." Na tena, "Tazama, hapa nipo na watoto ambao Mungu amenipa." 14 Kwa
hiyo, kwa kuwa watoto wa Mungu wote hushiriki mwili na damu, kadhalika Yesu alishiriki vitu vilevile, ili
kwamba kupitia kifo apate kumdhohofisha yule ambaye ana mamlaka juu ya mauti, ambaye ni ibilisi. 15
Hii ilikuwa hivyo ili awaweke huru wale wote ambao kupitia hofu ya kifo waliishi maisha yao yote katika
utumwa. 16 Kwa hakika siyo malaika anaowasaidia. Badala yake, anawasaidia wazao wa Abraham. 17 Kwa
hiyo, ilikuwa lazima yeye awe kama ndugu zake katika njia zote, ili aweze kuwa kuhani mkuu mwenye
huruma na mwaminifu kwa vitu vya Mungu, na ili kwamba awe na uwezo wa kutoa msamaha kwa dhambi
za watu. 18 Kwa sababu Yesu mwenyewe ameteseka, na kujaribiwa, ana uwezo wa kuwasaidia wale
wanaojaribiwa.

---

## Waebrania 02 Maelezo kwa jumla

### Muundo na mpangilio

Sura hii inahusu jinsi Yesu ni bora kuliko Musa, Mwisraeli mkuu kuliko wote.

Watafsiri wengine wameweka kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 2:6-8, 12-13, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Ndugu

Huenda mwandishi anatumia neno "ndugu" kuashiria Wakristo waliokua kama Wayahudi.

---

### Hebrews 2:1

**Sentensi Unganishi:**
Hili ni onyo la kwanza kati ya maonyo matano mwandishi anatoa

**Ni lazima**
Hapa "sisi"inamaanisha mwandishi anajijumuisha kwenye kundi lake.

**ili kwamba tukatengwa/ kuchukuliwa mbali**
kuamini katika neno la Mungu kidogo huongelewa kana kwamba mtumbwi ulikuwa ukichukuliwa mbali juu ya maji kutoka mahali ulipaswa kuwa. AT: " ili kwamba polepole tusiache kuliamini."

## Hebrews 2:2

**Kama ujumbe uliozungumzwa kupitia malaika**
Wayahudi waliamini kuwa Mungu alisema sheria yake kupitia malaika. Hii inaweza kuelezewa katika mfumo tendaji. AT: "Kama ujumbe ambao Mungu aliongea kupitia malaika"

**Kwa kuwa kama ujumbe**
Mwandishi ana hakika kuwa mambo haya ni kweli. AT: "Kwa sababu ujumbe"

**Ni halali**
"ni sahihi au "kweli"

**kila kosa na uasi hupokea adhabu ya haki**
Neno kosa and uasi husimama kwa ajili ya watu ambao wana hatia kwa ajili ya dhambi hizi. AT: "kila mtu atendaye dhambi atapokea adhabu ya haki"

**kosa na uasi**
maneno haya mawili kimsingi yanamaanisha kitu kimoja.

**tutapataje kuepuka kama tusipojali wokovu mku u kama huu?**
Mwanadishi anatumia swali kusisitiza watu wata pokea adhabu kama watakataa wokovu wa Mungu kupitia Kristo. AT: "hivyo Mungu atatuadhibu kama hatuutilii manani ujumbe wake kuhusu vile Mungu atakavyo tuokoa!"

**kutojali**
"kutojali" au "kuona sio muhimu"

**Huu ni waovu ambao kwanza ulitangazwa na Bwana**
Hii inaweza kusemwa katika mtumo tendaji. AT: "Bwana mwenyewe kwanza alitangaza ujumbe vile atakavyo tuokoa"

**na amethuthibitishia kupitia wale walio sikia**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. " na wale walio siki ujumbe walituthibitishia"

**kulingana namapenzi yake**
" kama jinsi alivyopenda kufanya"

## Hebrews 2:5

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anawakumbusha Waebrania hawa kwamba siku moja nchi itakuwa chini ya utawala wa Bwana Yesu.

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hapa inatoka katika kitabu cha Zaburi katika Agano la Kale. Inaendele hadi sehemu inayofuata.

**Kwa sababu kama haikuwa kwa malaika ambao Mungu aliwaweka**
"Kwa kuwa Mungu hakuwaweka malaika kuwa watawala"

**Ulimwengu ujao**
"Ulimwengu" hapa unamaanisha kwa watu wanaoishi huko. Na "ujao" unamaanishi huu ni ulimwengu uajao baada ya Yesu atakaporudi. AT: "watu watakaoishi katika ulimwengu wa mpya"

**Mtuni nani, kwamba uweze kumkumbuka/ kumjali?**
Swali linatumika kusisitiza kuwa wanadamu sio muhimu kwa kumfanya Mungu kuwajal.AT: "Hakuna mwandamu ambaye ni wa Muhimu wa kumfanya Mungu kufikiri kuhusu yeye!"

**Au mwana wa mtu , kwamba umjali?**
Kimsingi hii inamaanisha kitu kilekile kinachoelezewa katika swali la kwanza. Swali lisilo hitaji kujibiwa linasisitiza mshangao kwamba wanadamu si wa muhimu kiasi cha kwamba Mungu awajalli.AT: "Hakuna mwanadamu anayesitahili kujaliwa na wewe!"

## Hebrews 2:7

**mdogo kuliko malaika**
Mwandishi anamuongelea mwanadamu kuwa sio wa muhimu kuliko malaika kana kwamba wanadamuwamesimama katika nafasi amabayo ni ya chini kuliko nafasi ya malaika. AT: "mdogo kuliko malaika."

**amemfanya mtu...amevika... miguu yake... kwake**
Maneno haya sio kwa ajili ya mlengwa mmoja bali inajumuisha wanadamu wote, inajumuisha wanaume na wanawake.AT: "amewafanya wanadamu... amewavika...miguu yao... kwao"

**umemvika utukufu na heshima**
zawadi ya utukufu na heshima zinaongelewa kana kwamba ni shada la majani lililowekwa kichwani mwa mshindi wa mchezo. AT:"umewapa utukufu mwing na heshima"

**Umeweka kila kitu kiwe chini ya miguu yake**
Mwandishi anamuongelea mwanadamu kuwa na utawala juu ya kila kitu kana kwamba wamesimama juu ya kila kitu. AT: "Umewapa kumiliki juu ya vitu vyote"

**Hakuacha kitu chochote kisicho kuwa chini yake**
maneno mawili hasi yanamaanisha kwamba vitu vyote vitawekwa chini ya Kristo. AT: "Mungu alifanya kila kitu kuwa chini yao"

**Hatuoni vitu vyote vikiwa chini yake**
tunafahamu kuwa bado wanadamu hawajawa wamiliki wa kila kitu

## Hebrews 2:9

**Sentensi Unganishi:**
Mwanadishi anawakumbusha hawa Webrania waumini kwamba Kristo alipokuaja duniania alifanyika mdogo kuliko malaika alipokuja dunia

kuteseka kufa kwa ajili ya msamaha wa dhambi, na kwamba alifanyika kuhani mkuu mwenye huruma.

**tunamwona ambaye**
"twafahamu kuwa kuna mwingine"

**aliyefanyika**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji.AT: "ambaye Mungu alimfanya'

**chini kuliko malaika...amevikwa utukufu na heshima**
Tasifri hii kama ulitafsiri sura ya 2:7

**amevikwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mungu alimvika'

**amaeonja kifo**
Uzoefu wa kifo unaongelewa kana kwamba kifo ni chakula kilichoonjwa.AT: "ameonja kifo" au "amekufa"

**kwa kuwa kila mtu**
"Mtu" hapa linamaanisha watu wote. wakijumuishwa wanaume na wanawake. AT: "kwa kuwa kila mtu"

**awaleta wana wengi katika utukufu**
Zawadi ya utukufu hapa inaongelewa kana kwamba ni sehemu ambayo watu wangeweza kuletwa. AT: "awaokoe wana wengi"

**wana wengi**
Hapa wanamaanishwa waumini wote katika Kristo, ikijumuisha wanaume na wanawake.AT: "waumini wengi"

**kiongozi wa wokovu wao**
Mwanadishi anaongea wokovu kana kwamba ni sehemu ambayo Yesu anawaongoza waumini kuelekea katika sehemu hiyo. Hii inamaanisha Yesu ni mtu ambaye alitenda kwanza ili awaokoe wengine. AT:"yeye anayewaokoa watu"

**mkamilifu/ timiza**
kukua kiroho na kufundishwa kikamilifu kunaongelewa kana kwamba mtu alikuwa akifanywa mtimilifu, pengine mtimilifu katika viungo vya mwili wake.

## Hebrews 2:11

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii ya kinabii inatoka katika Zaburi ya Mfalme Daudi.

**yeye anaye dhabihu**
yeye anayewafanya wenzake watakatifu" au " "yeye awafanyae wengine kujtenga na dhambi"

**walio takaswa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji: AT: "wote anao wafanya watakatifu" au" wale anaowasafisha kutoka katika dhambi.

**kuwa na chanzo kimoja**
ambaye ni chanzo hicho ni nani inaweza kusemwa kwa ufasaha. AT: "muwe na chanzo, Mungu mwenyewe" au" muwe na yule yule.

**haoni aibu**
"Yesu haoni aibu"

**haoni aibu kuwaita ndugu**
maneno mawili hasi yanamaanisha atawafanya kama ndugu zake. AT: "anafurahishwa kuwaita ndugu"

**Nitalitangaza jina langu kwa ndugu zangu**
"Jina" hapa linamaanisha heshima ya mtu na kile walichokifanya. AT: "Nitatangaza kwa ndugu zangu mambo makuu uliyoyafanya"

**kutoka katika asili/ kundi moja**
"wakati waumini wanakuja pamoja kumwabudu Mungu"

## Hebrews 2:13

**Maelezo Jumla:**
Nabii Isaya aliandika nukuu hizi

**Na tena**
"Na nabii aliandika andiko katika sura nyingine kuhusu kileKristo achokisema kuhusu Mungu:" (URD)

**watoto... watoto wa Mungu**
Hii inaongea wale wanaoamini katika Kristo kana kwamba ni walikuwa watoto wa Mungu.AT: wale walio kama watoto wangu...wale ambaao ni sawa na watoto kwa Mungu"

**waliishi maisha yao yote katika utumwa.**
Fungu hili la maneno limeelezwa na hurejea utumwa kwa hofu ya kifo

**wanashiriki damu na mwili**
maneno "mwili" na "damu" inamaanisha asili ya wanadamu." AT: "wote ni wanadamu"

**"Yesu pia alishiriki mambo hayo hayo"**
"Yesu alikuwa mwanadamu kama wao"

**kwa kupitia kifo**
kifo hapa kinaweza kuelezewa kama tendo. AT: "kwa kufa"

**"alikuwa na nguvu ya kifo**
kifo" hapa kinaweza kuelezewa kama tendo.AT: " alikuwa na kuvungu kuwafanya watu kufa"

**Hii ilikuwa ili kwamba aweze kuwafanya huru wale wote ambao kupitia hofu ya kifo waliishi maisha ya utumwa**
Hofu ya kifo inaongelewa kana kwamba ilikuwa utumwa. Kumuondolea mtu hofu inaongelewa kana kwamba ni kumfungua mtu kutoka utumwani.AT: "Hii ilikuwa ili kwamba awafungue watu wote. Kwa

sababu tuliishi kama watumwa kwa sababu tulikuwa tukiogopa kufa"

### Hebrews 2:16

**mbegu ya Ibrahimu**
Wana wa Ibrahimu wanaongelewa kana kwamba walikuwa mbegu yake. AT: "wana wa Ibrahimu"

**ilikuwa ni muhimu kwake**
"ilikuwa ni muhimu kwa Yesu"

**kama ndugu zake**
Neno "ndugu" hapa linamaanisha watu kwa ujumla. AT: "kama wanadamu"

**ili alete msamaha wa dhambi kwa watu**
Kifo cha Yesu msalabani kinamaanisha kwamba Mungu anaweza kusamehe dhambi. AT: "ili kwamba afanye uwezekano wa Mungu kusamehe dhambi za watu."

**alijaribiwa**
Hii inaweza kusema katika mfumo tendaji. AT: " Shetani akamjaribu"

**wanaojaribiwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "ambao shetani anawajaribu"

---


generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Chapter 3

1 Kwa hiyo, ndugu watakatifu, washiriki wa wito wa mbinguni, mumfikiri Yesu, Mtume na Kuhani Mkuu
wa ukiri wetu. 2 Alikuwa mwaminifu kwa Mungu aliyemteua, kama Musa alivyokuwa mwaminifu pia
katika nyumba yote ya Mungu. 3 Kwa kuwa Yesu amehesabiwa kuwa na heshima kubwa kuliko aliyokuwa
nayo Musa, kwa sababu yule anayejenga nyumba anahesabiwa kuwa na heshima kubwa kuliko nyumba
yenyewe. 4 Kwa kuwa kila nyumba hujengwa na mtu fulani, lakini yule anayejenga kila kitu ni Mungu. 5
Hakika Musa alikuwa mwaminifu kama mtumishi katika nyumba yote ya Mungu, akitoa ushuhuda kuhusu
mambo yatakayosemwa wakati ujao. 6 Lakini Kristo ni Mwana katika usimamizi wa nyumba ya Mungu.
Sisi ni nyumba yake kama tutashikilia haraka katika kujiamini na fahari ya kujiamini. 7 Kwa hiyo, ni kama
Roho Mtakatifu asemavyo, "Leo, kama utasikia sauti yake, 8 Usiufanye moyo wako kuwa mgumu kama
Waisraeli walivyofanya katika uasi, katika wakati wa kujaribiwa nyikani. 9 Huu ulikuwa wakati ambao
baba zenu waliniasi kwa kunijaribu, na wakati, kwa miaka arobaini, waliona matendo yangu. 10 Kwa hiyo
sikufurahishwa na kizazi hicho. Nilisema, 'Wanapotea kila mara katika mioyo yao, na hawajui njia zangu.
11 Ni kama vile nilivyoapa katika hasira yangu: hawataiingia raha yangu." 12 Muwe waangalifu, ndugu, ili
kwamba usije ukawepo moyo mwovu wa kutokuamini kwa mmoja wenu, moyo ambao utakwenda mbali na
Mungu aliye hai. 13 Badala yake, mhamasishane kila siku kila mmoja na mwenzie, ili kila iitwapo leo
mtamani, ili kwamba mmoja kati yenu asifanywe kuwa mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. 14 Kwa
maana tumekuwa washiriki wa Kristo ikiwa tutashikamana na uthabiti wetu kwa nguvu katika yeye
kutoka mwanzo hadi mwisho. 15 Kuhusu hili imekwisha kusemwa, "Leo kama mtaisikiliza sauti yake,
msiifanye mioyo yenu kuwa migumu, kama Waisraeli walivyofanya wakati wa uasi." 16 Ni akina nani hao
waliomsikia Mungu na kuasi? Hawakuwa wale wote ambao Musa alikuwa amewaongoza kutoka Misri? 17
Na kina nani ambao Mungu aliwakasirikia kwa miaka arobaini? Siyo pamoja na wale waliotenda dhambi,
ambao miili yao iliyokufa ililala jangwani? 18 Ni akina nani aliowaapia Mungu kwamba hawataingia katika
raha yake, kama siyo wale ambao hawakumtii yeye? 19 Tunaona kwamba hawakuweza kuingia katika
raha yake kwa sababu ya kutokuamini.

---

## Waebrania 03 Maelezo kwa jumla

### Muundo na mpangilio

Watafsiri wengine wamewaka kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 3:7-11,15, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Ndugu

Huenda mwandishi anatumia neno "ndugu" kuashiria Wakristo waliokua kama Wayahudi.

### Mifano muhimu za usemi katika sura hii

### Fanya mioyo yenu iwe ngumu

Mtu anayefanya moyo wake kuwa ngumu ni yule ambaye hatamsikiliza ama kumtii Mungu.

### Maswali ya hadith

Mwandishi anatumia maswali ya hadithi kama njia ya kuwaonya wasomaji wake. Yeye pamoja na wasomaji wake wanajua majibu ya maswali haya na mwandishi anajua kwamba wakati wasomaji watafikiria juu ya majibu ya haya maswali, watatambua kwamba wanatakikana kumsikiliza Mungu na kumtii.

---


generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Hebrews 3:1

**Sentensi Unganishi:**
Hili ni onyo la pili na ni refu na liko katika undani na linajumuisha sura ya 3 na 4. Mwandishi anaanza kwa kwa kuonyesha kwamba Kristo ni bora zaidi ya Musa mtumishi wake.

**ndugu watakatifu**
Neno "ndugu" linamaanisha wakristo wenza, inajumuisha wanaume kwa wanawake. AT: "kaka na dada watakatifu" au "ndugu watakatifu wenzangu"

**mnashirika katika mwito wa mbinguni**
"Mbinguni" hapa ina mwakilisha Mungu. AT: "Mungu ametuita pamoja"

**mtume**
Neno hili linamaanisha mtu aliyetumwa. Katika kifungu hiki hakimaanishi mtume kati ya wale kumi na wawili. AT: "aliyetumwa"

**ya ukiri wetu**
hii inaweza kusemwa ili kwamba nomino dhaniwa "kutubu" inelezea kama kitenzi "tubu." AT: "ambaye tunayemtubia" au "ambaye katika yeye tunaamini"

**katika nyumba ya Mungu**
Waebrania ambao Mungu amejifunua kana kwamba ilikuwa ni nyumba halisi. AT: "kwa watu wote wa Mungu"

**Yesu amefinywa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mungu amemfanya Yesu"

**yeye ajengaye kila kitu**
Matendo ya Mungu ya uumbaji wa ulimwengu yanaongelewa kana kwamba amejenga nyumba.

**kila nyumba imejengwa na mtu**
Hii inaweza kuelezwa katika mfumo tendaji. AT: "kila nyumba ina mtu aliyeijenga"

## Hebrews 3:5

**Hakika/ na**
Hili neno linaanzishwa ulinganifu kati ya Musa na Kristo. Hili neno linaweza kuachwa katika tafsiri, kama sio muhimu.

**Katika nyumba nzima ya Mungu**
Waebrania ambao Mungu alijifunua mwenyewe wanaongelewa kana kwamba zilikuwa ni nyumba halisi. Tazama vile ulivyo tafasiri kama ulivyofanya 3:1.

**Alikuwa ni ushuhuda kuhusu vitu**
Pengine neno hili linamaanisha kwa kazi zote za Musa. AT: "Maisha na kazi za Musa zilielekeza kwenye vitu"

**Viliongelewa katika wakati ujao**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: " Yesu angesema katika siku zijazo"

**Mwana**
Hiki ni cheo muhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu.

**mtumishi katika nyumba ya Mungu**
Hii inaongea kuhusu watu wa Mungu kana kwamba zilikuwa nyumba halisi. AT: "ambaye anatawala juu ya watu wa Mungu"

**Sisi ni nyumba yake**
Hii inaongea kwa watu wa Mungu kana kwamba ni nyumba halisi. AT: "Sisi ni watu wa Mungu"

**kama tukiendelea kushikilia "ujasiri" wetu na tumaini letu lenye fahari**
"ujasiri" na "tumaini lenye fahari" ni dhaaniwa na inaweza kusemwa kama vitenzi. AT: "tutaendelea katika ujasiri na furaha na kutumaini Mungu kufanya kile alichoahidi"

## Hebrews 3:7

**Sentensi Unganishi:**
Onyo hapa ni ukumbusho kwamba kutokuamini kwa Waisraeli kuliwafanya wote kutoingia katika nchi ambayo Mungu alikuwa amewahidi. Kutokuamini kwao kulionyeshwa vizuri katika Kutoka 17:1, walipo mlalamikia Musa na kuwa na mashaka juu ya Mungu kama alikuwa pamoja nao.

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii inatoka katika Agano la Kale katika Zaburi.

**kama mkisikia sauti yake**
Amri za Mungu kwa Waisraeli zinaongelewa kana kwamba aliwakuwa amewapa katika sauti ya kusikika. AT: "kama mtasikia Mungu akiongea"

**Msifanye mioyo yenu kuwa migumu**
Ugumu wa moyo unaongelewa kana kwamba ni moyo halisi umefanywa kuwa mgumu. AT: "msiwewenye mioyo migumu"

**kama katika uasi wakati wa kujaribiwa jangwani**
Hapa "uasi" na "kujaribiwa" yanaweza kuelezewa kama vitenzi. AT: "kama vile na mababu zenu walivyo muasi Mungu na kumjaribu jangwani"

## Hebrews 3:9

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii inatoka katika Zaburi.

**Mababa**
"zenu" hapa linamaanisha watu wa Israeli

**kwa kunijaribu**
Mungu ndiye anayeongea

**miaka arobaini**
"miaka 40"

**Sikufurahishwa**
"Nilikuwa na hasira" au "sikufurahia kabisa"

**mara zote wanapotoshwa katika mioyo yao**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "mara zote wanaenda katika njia zisizomfurahisha Mungu"

**mioyoni mwao**
Neno "mioyo" inamaanisha akili au tamaa za

**Wamevijua njia zangu**
Hii inaongelewa katika hali ya kuyafanya maisha ya mtu kana kwamba ni zilikuwa ni njia. AT: "Hawaelewi jinsi nilivyowataka waishi katika maisha yao"

**Hawataingia katika pumziko langu**
Amani na ulinzi uliotolewa na Mungu unaongelewa kana kwamba zilikuwa pumziko ambalo angeweza kuwapa, na kama zilikuwa ni sehemu ambayo watu wangeweza kwenda. AT: "Hawataingia kamwe katika sehemu ya pumziko" au "sitawaruhusu kupata baraka zangu za pumziko"

## Hebrews 3:12

**ndugu**
Hili linatulejesha kwa ndugu Wakristo, ikijumuisha jinsia zote mbili za kiume na kike. AT: "kaka na dada" au "waumini wenza"

**Hakutakuwa na mtu yeyote aliye na moyo mwovu usioamini**
moyo unaongelewa hapa kana kwamba ni akili ya mtu, sehemu ya utashi ya mtu. AT: "mtu yeyote kati yenu asiache kuamini katika Mungu"

**Moyo ambao unageuka kinyume na Mungu**
Moyo mtu unaongelewa kana kwamba nimtu mzima, ambaye angeweza kuacha kufuata njia sahihi. AT: "na unaacha kumtii Mungu aishie"

**Mungu aishie**
"Mungu wa kweli ambaye kweli anaishi"

**kama iitavyo "leo"**
"wakati nafasi inapatikana"

**Hakuna mmoja miongoni mwenu moyo wake utfanywa mgumu kwa udanganyifu wa dhambi.**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "udanganyifu wa dhambi haufanyi moyo mgumu wa mtu yeyote kati yenu"

**hakunammoja kati yenu moyo wake utafanywa kuwa mgumu kwa udanganyifu wa dhambi**
kutokuwa msikivu kunatazamwa kana kwamba kuwa mgumu au kuwa na moyo mgumu. Ugumu wa moyo ni matokeo ya udanganyifu wa dhambi. Hii inaweza kutiwa neno ili kwamba nomino dhaniwa "udanganyifu" inaelezewa kama kitenzi "danganya." AT: "hakuna mtu miongoni mwenu atanganywa na dhambi na kutokuwa msikivu" au "usitende dhambi, ukijidanganya mwenyewe na kutokuwa msikivu"

## Hebrews 3:14

**Maelezo ya Jumla:**
Hii inaendelea kutoka Zaburi ile ile ambayo pia ilinukuliwa katika 3:7.

**Kwa sababu tumekuwa**
"Tumekuwa" hapa inamaanisha wote, mwandishi na wasomaji,

**kama tutaendelea kushikilia ujasiri wetu katika yeye**
"kama tukiendelea kutumaini katika yeye kwa ujasiri"

**kutoka mwanzo**
"tangu mwanzo tulipoanza kuamini katika yeye"

**hadi mwisho**
Hii ni namna ya kusema kwa upole ikimaanisha mtu anapo kufa.AT: "hadi tunakufa"

**imesemwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "mwandishi aliandika"

**Leo, ukisikia**
Amri ya Mungu kwa Waisraeli zinaongelewa kana kwamba aliwapa katika hali ya kusikia. AT: "kama utasikia Mungu anaongea." Tazama kama ulivyo tafsiri 3:7.

**kama katika kuasi**
"Uasi" hapa unaweza kusemwa kama kitenzi. AT: "kama vile mababa zako walivyo muasi Mungu." Tanzama ulivyo tafsiri 3:7.

## Hebrews 3:16

**Maelezo ya Jumla:**
Neno "wao" linamaanisha kwa kutotii kwa Waisraeli, na "sisi" inamaanisha mwandishi na wasomaji.

**Ni wakina nani walio msikia Mungu na kuasi? Si wale waliokuja kutoka Misri kupitia Musa?**
Mwandishi anatumia maswali kudundisha wasomaji wake. Maswali haya mawili yanaweza kuunganishwa kama sentensi moja, kama itahitajika. AT: "wale wote waliokuja na Musa kutoka Misri walimsikia Mungu, lakini bado waliasi."

**Ni akina nani ambao Mungu aliawakasirikia kwa miaka arobaini? Sio wale waliotenda dhambi, ni miili ya kina nani iliyanguka jangwani/ nyikani?**
Mwandishi anatumia maswali kuwafundisha wasomaji wake. Maswali haya mawli yanaweza kuunganishwa na kuwa swali moja, kama

litahitajika. AT: "Mungu alikuwa na hasira kwa miaka 40 na wale waliotenda dhambi na kuwaacha wafe nyikani."

**hawakuweza kuingia katika raha yake**
Amani na ulinzi ambao Mungu vinaomgelewa kana kwamba ni pumziko alilowapa, na kama kwama vilikuwa ni sehemu za kwenda. AT: "hawataingia sehemu ya pumziko" au "hawatapata baraka zake za pumziko"

**kwa sababu ya kutokuamini kwao**
"kutokuamini" inaweza kusemwa kama kitenzi "tumaini." AT: "kwa sababu hawakuweza kumtumaini"

## Chapter 4

1 Kwa hiyo, tunapaswa kuwa makini ili kwamba kati yenu asiwepo hata mmoja atakayeonekana kushindwa kufikia ahadi endelevu ya kuingia katika pumzika la Mungu. 2 Kwani tumekuwa na habari njema kuhusu pumziko la Mungu lililotangazwa kwetu kama Waisrael walivyokuwa nayo, lakini ujumbe huo haukuwasaidia wale ambao waliusikia bila kuunganisha imani kwa hilo. 3 Kwa sisi, ambao tumekwisha amini-sisi ndio miongoni tutakaoingia katika lile pumuziko, Kama inavyosema, "Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia katika pumziko mwangu." Alisema hili, ingawa kazi zote alizotengeneza zilikuwa zimekamilika tangu mwanzo wa ulimwengu. 4 Kwani ameshasema sehemu fulani kuhusu siku ya saba, "Mungu alipumzika siku ya saba katika yote aliyoyafanya." 5 Tena ameshasema, "Hawataingia kwenye pumziko langu." 6 Kwa sababu hiyo, tangu pumziko la Mungu bado ni akiba kwa ajili ya baadhi kuingia, na tangu Waisraeli wengi ambao walisikia habari njema kuhusu pumziko lake hawakuingia kwa sababu ya kutotii, 7 Mungu aliweka tena siku fulani, iitwayo "Leo." Yeye aliiongeza siku hii alipozungumza kupitia Daudi, ambaye alisema kwa muda mrefu baada ya yaliyosemwa kwanza, "Leo kama mtasikia sauti yake, msifanye mioyo yenu kuwa migumu." 8 Kwani kama Yoshua aliwapatia pumziko, Mungu asingelisema juu ya siku nyingine. 9 Kwa hiyo bado kuna Sabato ya pumziko iliyotunzwa kwa ajili ya watu wa Mungu. 10 Kwani anayeingia katika pumziko la Mungu yeye mwenyewe pia amepumzika kutokana na matendo yake, kama Mungu alivyofanya katika yeye. 11 Kwa hiyo tuweni na shauku ya kuingia katika lile pumziko, ili kwamba asiwepo atakayeanguka katika aina ya uasi waliofanya. 12 Kwa maana neno la Mungu li hai na lina nguvu na linaukali kuliko upanga wowote wenye makali kuwili. Na huchoma hata kufikia kugawanya nafsi na roho, na viungo kutika uboho. Na lenye kuweza kufahamu fikira za moyo nia yake. 13 . Hakuna kilichoumbwa kilichojificha katika uso wa Mungu. Badala yake, kila kitu ni dhahiri na wazi kwa macho ya mmoja ambaye ni lazima tutoe hesabu. 14 Baadaye kuwa na kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu, kwa uimara tushikilie imani zetu. 15 Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu ambaye hawezi kuhisi huruma kwa ajili udhaifu wetu, lakini yeye ambaye kwa njia zote amekuwa akijaribiwa kama sisi, isipokuwa yeye ambaye hana dhambi. 16 Na tuje kwa ujasiri katika kiti cha enzi cha neema, ili kwamba tupokee rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa hitaji.

---

## Waebrania 04 Maelezo kwa jumla.

### Muundo na mpangilio

Sura hii inaelezea kwa nini Yesu ni Kuhani Mkuu kuliko wote

Watafsiri wengine wametenga kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 4:3-4,7, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Mapumziko ya Mungu

Neno "mapumziko" linaonekana kuashiria vitu viwili katika sura hii. Inaashiria mahali ama wakati Mungu atawaruhusu watu wake kupumzika kutokana na kazi zao (Waebrania 4:3), ama inaashiria kupumzika kwa Mungu siku ya Saba (Waebrania 4:4).

---

### Hebrews 4:1

**Sentensi Unganishi**

Sura ya 4inaendeleza onyo lililoanza katika sura ya 3:7.Mungu kwa kupitia mwandishi anawapa waumini pumziko ambalo pumziko la Mungu katika uumbaji dunia ni picha.

**kati yenu asiwepo hata mmoja atakayeweza kuonekana kushindwa kuifikia ahadi ya kuingia katika pumziko la Mungu iliyobaki kwa ajili yenu**

Ahadi ya Mungu inaongelewa kana kwamba ilikuwa ni zawadi iliyoachwa baada ya Mungu kuwatembelea watu. AT: "mmoja wenu asishindwe kuingia katika pumziko la Mungu , ambalo alituahidi".



generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

**kuingia katika pumziko la Mungu**
Amani na ulinzi uliotolewa na Mungu huongelewa kana kwamba vilikuwa ni pumziko ambalo anaweza kuwapa, na kana kwamba vilikuwa ni sehemu ambayo watu wangeweza kwenda. AT: "kuingia katika sehemu ya pumziko" au "kupata baraka za pumziko la Mungu.

**Kwani tumekuwa na habari njema kama walivyokuwa nazo**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Kwa kuwa tulisikia habari njema kama walivyosikia"

**kama walivyo**
walivyo hapa linamaanisha mababu/mababa wa Kiebrania ambao walikuwa hai wakati wa Musa.

**Lakini ujumbe ule haukuwafaa wale ambao hawakuungana katika imani pamoja na wale walio tii**
"Lakini ujumbe ule haukuwafaa wale ambao hawakuungana na watu walio amini na kutii." Mwandishi anaongea kuhusu makundi mawili ya watu, wale waliopokea agano la Mungu kwa imani, na wale walio sikia lakini hawakuamini.

## Hebrews 4:3

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu ya kwanza hapa (Kama nilivyoapa...) inatoka katika Zaburi, na nukuu ya pili (Mungu akapumzika...) inatoka katika Maandiko ya Musa, na ya tatu (Hawataingia...) inatoka katika Zaburi.

**Sisi tulioamini**
"sisi tulioamini"

**watakao ingia katika pumziko hilo**
Amani na ulinzi alioutoa Mungu vinaongelewa kana kwamba vilikuwa ni pumziko ambazo anaweza kuwapa, na kana kwamba ilikuwa ni sehemu ambayo watu wangeenda.

**Kama alivyo sema**
"Kama vile Mungu alivyosema"

**Kama nilivyo apa katika hasira yangu**
"Kama nilivyo apa wakati nilipokuwa nimekasirika sana"

**Hawataingia kwenye pumziko langu**
Amani na ulinzi uliotolewa na Mungu vinaongelwa kana kwamba zilikuwa pumziko la kuwapa, na kana kwamba vilikuwa ni sehemu ambayo watu wangeweza kwenda.

**kazi yake ya uumbaji ilimalizika**
Hii inaweza kuwekwa katika mfumo tendaji. AT: "alimaliza uumbaji" au "alimaliza kazi zake za uumbaji"

**tangu mwanzo wa dunia/ ulimwengu**
Mwandishi anaongelea dunia kana kwamba ni jengo lililowekwa kwenye kwenye msingi.

**siku ya saba**
Hii inasimama kama badala ya "saba"

## Hebrews 4:6

**bado imewekwa kwa baadhi kuingia katika pumziko**
Amani na ulinzi uliotolewa na Mungu vinaongelwa kana kwamba zilikuwa pumziko la kuwapa, na kana kwamba vilikuwa ni sehemu ambayo watu wangeweza kwenda. Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji.AT: "Mungu bado anaruhusu baadhi ya watu kuingia katika sehemu yake ya pumziko.

**kama mtasikia sauti yake**
Amri za Mungu kwa Waisraeli zinaongelewa kana kwamba alikuwa amewapa kwa sauti. AT: "kama mtasikia Mungu akiongea"

**msifanye mioyo yenu kuwa migumu**
kutosikia kunaongelewa kana kwamba ni moyo ulikuwa umwefanya kuwa mgumu. AT: "Msiwe wenye mioyo migumu." Tafsiri kama ulivyofanya 3:7.

## Hebrews 4:8

**Sentensi Unganishi:**
Mwanadishi anawaonya waumini wasiache kumtii Mungu, bali waiingie katika pumziko ambalo Mungu anawapa. Anawakumbusha kwamba neno la Mungu litawashuhudia na kwamba wanaweza katika maombi kwa ujasiri na kwamba Mungu atawasaidia

**kama Yoshua angekuwa amewapa pumziko**
Amani na ulinzi uliotolewa na Mungu vinaongelwa kana kwamba zilikuwa pumziko la kuwapa, na kana kwamba vilikuwa ni sehemu ambayo watu wangeweza kwenda. AT: "kama Yoshua angewaleta Wasraeli kwenye sehemu ambayo Mungu angewapa pumziko"

**tuwe na shauku**
Amani na ulinzi uliotolewa na Mungu vinaongelwa kana kwamba zilikuwa pumziko la kuwapa, na kana kwamba vilikuwa ni sehemu ya kuingia. AT: "tunapaswa kufanya kila kitu ili tuingie katika mpumziko mahali alipo"

**wataanguka katika aina ya kutotii ambao walifanya**
kutokutii kunaongelewa kana kwamba ni mtu mzima ambaye angeweza kuanguka katika ajali.

## Hebrews 4:12

**neno la Mungu li hai**
"Neno la Mungu" hapa linamaanisha kila kitu ambacho Mungu ameongea kwa wanadamu iwe kwa kuongea au kwa kupitia ujumbe ulioandikwa.

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

**lina hai na lina nguvu**
Hii inaongelea neno la Mungu kana kwamba linaishi. Inamaanisha wakati Mungu anapoongea ni kuna nguvu na utendaji kazi.

**lina ukali kuliko upanga wowote wenye makali mawili**
upanga wenye makali. upanga wenye makali kuwili ni rahisi kukata kupitia mwili wa mtu. Neno la Mungu lina nguvu katika kuonyesha kilichomo katika moyo na mawazo ya watu.

**Na huchoma hata kufikia kugawanya nafsi na roho, na viungo kutika uboho.**
Hii inaendelea kuongea kuhusu neno la Mungu kana kwamba ulikuwa ni upanga. Upanga hapa ni mkali sana kiasi kwamba unaweza kukata na kugawa viungo vya mwanadamu ambavyo ni vigumu pengine visivyo wezekana kugawanyika.

**nafsi na roho**
Haya ni maneno mawili tofauti lakini sehemu za mwanadamu ambazo hazina mwili. "Nafsi" ndiyo inamfanya mtu kuwa hai na "roho" ni sehemu ya mtu ambayo inamsababisha kuweza kumjua na kumwamini Mungu.

**viungo kutoka maboho**
"kiungo" ndicho kinacho shikilia mifupa miwili pamoja. "uboho" ni sehemu ya kati ya mfupa.

**kuweza kufahamu**
Hii inaongea neno la Mungu kana kwamba ni mtu ambaye angewezakujua kitu.

**mawazo na makusudi ya moyo**
Hii inaongea kuhusu moyo kana kwamba ni sehemu ya kati ya mawaazo na hisia za mwanadamu.

**Hakuna kilichoumbwa kilichojificha katika uso wa Mungu**
Hili linaweza kuelezwa katika mfumo tendaji. AT: "hakuna kitu kilichoumbwa na Mungu kinaweza kujificha mbele zake"

**kila kitu kiko wazi**
Hii inaongelea kila kitu kana kwamba ni mtu amesimama wazi au boksi lililo wazi.

**wazi na iliyo wazi**
Kimsingi maneno haya mawilii yanamaanisha kitu kimoja na kusisitiza kwamba hakuna kitu chochote kilichojificha mbele za Mungu.

**kwa macho ya yule tutakaye toa hesabu**
Mungu anaongelwa kana mwamba ana macho ya nyama. AT" Mungu atatuhukumu kulingana na vile tulivyoishi"

## Hebrews 4:14

**aliyeziingia mbingu**
"aliyeingia mahali alipo Mungu"

**Mwana wa Mungu**
Hiki ni cheo muhimu kwa Yesu.

**tushikilie sana imani zetu**
imani na tumaini vinaongelewa kana kwamba ni vitu ambavyo mtu angeweza kuvikumbatia.

**hatuna kuhani mkuu ambaye hawezi kutuhurumia... Badala, tunaye**
Maneno haya yakukanusha yanalenga kuonyesha kwamba Yesu ni mwenye huruma kwa watu . AT: " tunaye kuhani mkuu anayeweza kutuhurumia...Kweli tunaye"

**kiti cha enzi cha neema**
"kiti cha enzi cha Mungu, pale palipo na neema" au "pale Mungu, ambaye ni neema, ameketi katika kiti chake cha enzi"

**yeye ambaye kwa njia zote amekuwa akijaribiwa kama sisi**
Hii inaweza kusemwa katikamfumo tendaji. AT: "yeye ambaye amevumilia majaribu katika kila hali tunayoipitia" au "ambaye movu amekuwa akimjaribu katika kila njia anavyotujaribu"

**hana dhambi**
"hakutenda dhambi"

**kiti cha enzi cha neema**
"kwemye kiti cha enzi cha Mungu palipo na neema." "kiti cha enzi" hapa kina maanisha utawala wa Mungu kama mfalme.

**ili kwamba tupokee rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa hitaji.**
"rehema" na "neema" hapa vinaongelewa kana kwamba ni vitu ambavyo vinaweza kupewa au kupatikana.

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Chapter 5

1 Kwani kila kuhani mkuu, aliyechaguliwa kutoka miongoni mwa watu, amechaguliwa kusimama badala
yao katika vitu vinavyohusiana na Mungu, ili aweze kutoa kwa pamoja zawadi na dhabihu kwa ajili ya
dhambi. 2 Anaweza kujishughulisha kwa upole na wajinga na wabishi kwa kuwa yeye mwenyewe pia
amezungukwa na udhaifu. 3 Kwa sababu ya hili, ana wajibu wa kutoa sadaka kwa ajili ya dhambi zake
kama afanyavyo kwa dhambi za watu. 4 Na hakuna mtu achukuaye heshima hii kwa ajili yake mwenyewe,
lakini badala yake, lazima aitwe na Mungu, kama alivyokuwa Haruni. 5 Hata Kristo hakujipa heshimu
mwenyewe kwa kujifanya mwenyewe kuwa kuhani mkuu. Badala yake, Mungu alisema kwake, " Wewe ni
mwanangu, leo nimekuwa Baba yako." 6 Ni kama asemavyo pia sehemu nyingine, " Wewe ni kuhani milele
baada ya mfumo wa Melkizedeki." 7 Wakati wa kipindi chake katika mwili, aliomba na kuombea,
alimwomba Mungu kwa machozi, kwa yeye awezaye kumwokoa kutoka kwenye kifo. Kwa sababu ya
unyenyekevu wake kwa Mungu, alisikiwa. 8 Ijapokuwa alikua mwana, alijifunza kutii kwa mambo
yaliyomtesa. 9 Alikamilishwa na kwa njia hii alifanyika kwa kila mtu amwaminiye kuwa sababu ya wokovu
wa milele, 10 kwa kutengwa na Mungu kama kuhani Mkuu baada ya zamu ya Melkizedeki. 11 Tuna mengi
ya kusema kuhusu Yesu, lakini ni vigumu kuwaelezea kwa kuwa ninyi ni wavivu wa kusikia. 12 Ijapokuwa
kwa kipindi hiki mlipaswa kuwa walimu, bado kuna umuhimu wa mtu kuwafundisha mafundisho ya awali
ya kanuni za neno la Mungu. Mnahitaji maziwa na si chakula kigumu. 13 Kwa kuwa yeyote anywaye
maziwa tu hana uzoefu katika ujumbe wa haki, kwa kuwa bado ni mtoto. 14 Kwa upande mwingine,
chakula kigumu ni cha watu wazima, wale ambao kwa sababu ya uzoefu wao katika kutofautisha haki na
ubaya wamefundishwa kutambua jema na ovu.

---

## Waebrania 05 Maelezo kwa jumla

### Muundo na mpangilio

Sura hii inaendeleza mafundisho ya sura iliyopita.

Watafsiri wengine wametenga kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 5:5-6.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Kuhani mkuu

Ni kuhani mkuu tu angetoa dhabihu ili Mungu asamehe dhambi na kwa hivyo lazima Yesu alikuwa kuhani Mkuu. Sheria ya Musa iliamuru kwamba kuhani mkuu atoke kwa kabila la Walawi lakini Yesu alitoka kabila la Yuda.Mungu alimfanya kuhani kama Melikizedeki aliyeishi nyakati za Abarahamu kabla ya kuwepo kabila la Walawi.

### Mifano muhimu za usemi katika hi sura

### Maziwa na chakula kigumu

Mwandishi anazungumzia Wakristo ambao wako tu na uwezo wa kuelewa vitu rahisi kumhusu Yesu kana kwamba walikuwa watoto wachanga wanaokunywa tu maziwa na hawawezi kulaa chakula kigumu.

---

### Hebrews 5:1

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anafafanua dhambi za makuhani wa Agano la Kale, na kisha anaonyesha kuwa Kristo anao ukuhani bora, na hautokani na ukuhani wa haruni, bali unaotokana na ule waMelkizedeki.

**chaguliwa kutoka miongoni mwa watu**
Hii inaweza kusemwa katika muundo tendaji. AT: "ambaye Mungu anachagua kutoka miongoni mwa watu"

**amechaguliwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mungu huachangua/ huteuwa"


generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

**kusimama badala ya/ kutenda kwa niaba ya watu**
"kuwawakilisha watu"

**wajinga na waovu**
"wale walio wajinga waovu"

**waovu**
watu ambao wanaishi katika njia za dhambi"

**amezungukwa na udhaifu.**
udhaifu wa kuhani mkuu unaongelewa kana kwamba ni nguvu zilizo mzunguka

**udhaifu**
hapa inamaanisha hamu ya kutenda dhambi.

**pia anahitajika**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. "Mungu pia anamhitaji"

### Hebrews 5:4

**Sentensi Unganishi:**
Nukuu hii inatoka katika Zaburi katika Agano la Kale

**achukuaye heshima hii**
Heshima inaongelewa kana kwamba ni kitu ambacho Mungu kukichukua katika mkono wake.

**achukue heshima hii**
heshima au sifa na heshima ambazo watu walimpa kuhani mkuu husimama kwa ajili ya majukumu yake

**aitwe/ ameitwa na Mungu, kama alivyokuwa Haruni**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mungu alimwita kama alivyomwita Haruni"

**Mungu alisema kwake**
"Mungu alisema kwake"

**" Wewe ni mwanangu, leo nimekuwa Baba yako."**
kimsingi neno hili linamaanisha kitu kimoja. Tazama ulivyotafsiri 1:4.

### Hebrews 5:6

**Maelezo ya Jumla:**
Unabi huu unatoka katika Zabur ya Daudi.

**kama asemavyo/ pia anasema**
kwa yule ambaye Mungu anaongea naye inaweza kusemwa wazi. AT: "pia anamwambia Kristo"

**katika sehemu nyingine**
"katika sehemu nyingine katika maandiko"

**mfano wa Melkizedeki**
Hii inamaana kuwa Kristo kama kuhani ana vitu vinavyofanananana Melkizedeki kama kuhani.

### Hebrews 5:7

**kipindi chake katika mwili**
Neno siku/ kipindi zinasimama badala ya kipindi cha muda. Na "mwili" unasimama badala ya maisha ya Yesu duniani, AT: "wakati aliposhi duniani"

**maombi na kuombea/**
Kimsingi maneno haya yanamaanisha kitu kimoja

**kumwokoa kutoka kwenye kifo**
Kifo kinaongelewa kana kwamba ilikuwa ni sehemu kKristo angezuiliwa kutoingia, au kana kwamba ni sehemu ambayo angeokolewa.

**alisikiwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mungu alimsikia"

**mwana**
Hiki ni cheo muhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu.

**mambo yaliyomtesa**
mateso kana kwamba ni vitu.

### Hebrews 5:9

**Sentensi Unganishi:**
Katika mst wa11 mwandishi anaanza onyo lake la tatu. Anawaonya hawa wauminikuwa bado ni wachanga wa kiroho na kuwatia moyo kujjifunza neno la Mungu ili kwamba waweze kutambua jema na baya.

**alifanywa mkamilifu**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mungu alifanya mkamilifu"

**alifanya mkamilifu**
hapa inamaanisha kuweza kufanywa mtu mzima kiroho, kuwa tayari kumtii Mungu katika nyanja zote za maisha.

**Alikamilishwa na kwa njia hii alifanyika kwa kila mtu amwaminiye kuwa sababu ya wokovu wa milele**
Nomino dhaaniwa "wokovu" inaweza kusemwa kama kitenzi. AT: "hivyo anawaokoa wale wote wanaomtii na kuwafanya waishi milele"

**kwa kutengwa na Mungu**
Hii inaweza kusems katika mfumo tendaji. AT: "Mungu alimtenga" au "Mungu alimteua"

**baada ya zamu ya Melkizedeki**
hii inamaanisha kwamba Kristo kama kuhani ana vitu vinavyofanana na Melkizedeki kama kuhani.

**Tuna mengi ya kusema**
Ingawa mwandishi anatumia neno la wingi lakini inaweza kuwa anamaanisha yeye mwenyewe.

**ninyi ni wavivu wa kusikia**
uwezo wa kuelewa na kutii kunaongelewa kana kwamba ulikuwa ni uwezo wa kusikia. Na uwezo wa kusikia kunaongelewa kana kwamba ilikuwa ni chuma cha kilichohabika katika matumizi.

### Hebrews 5:12

**kanuni za msingi**
kanuni hapa zinamaanisha maelekezo au viwango vya kufanya maamuzi. AT:"msingi wa ukweli"

**Mnahitaji maziwa**
mafundisho kuhusu Mungu ambayo ni rahisi kuelewa yanaongelewa ni maziwa, chakula pekee ambacho watoto wachanga wanaweza kula. AT: "mmekuwa watoto na mnaweza kunywa maziwa pekee"

**si chakula kigumu**
mafundisho ambayo ni magumu kuelwa yanaongelewa kana kwamba kilikuwa ni chakula kigumu, kifaacho kwa watu wazima.

**anywaye maziwa**
anywaye linasimama ka kunywa.

**kwa sababu bado ni mtoto**
hii inaongelea waumni ambao wanaweza kuelewa mafundisho rahisi ya injili kana kwamba walikuwa watoto halisi.

**ambao kwa sababu ya uzoefu wao katika kutofautisha haki na ubaya wamefundishwa kutambua jema na ovu.**
watu walifundishwa kuelwa jambo wanaelezewa kana kwamba ni uwezo wa kuelewa umefundishwa.

---

## Chapter 6

1 Kwa hiyo, tukiacha tulichojifunza kwanza kuhusu ujumbe wa Kristo, twapaswa kuwa na juhudi kuelekea
kwenye ukomavu, tusiweke tena misingi ya toba kutoka katika kazi zisizo na uhai na imani katika Mungu,
2 wala misingi ya mafundisho ya ubatizo, na kuwawekea mikono, ufufuo wa wafu, na hukumu ya milele. 3
Na tutafanya hivi ikiwa Mungu ataruhusu. 4 Kwa kuwa haiwezekani kwa wale ambao waliipata nuru
awali, ambao walionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa kuwa washirika wa Roho Mtakatifu, 5 na
ambao walionja uzuri wa neno la Mungu na kwa nguvu za wakati ujao, 6 na kisha wakaanguka -
haiwezekani kuwarejesha tena katika toba. Hii ni kwa sababu wamemsulubisha Mwana wa Mungu mara
ya pili kwa nafsi zao, wakimfanya kuwa chombo cha dhihaka hadharani. 7 Kwa kuwa ardhi iliyopokea
mvua inyeshayo mara kwa mara juu yake, na ikatoa mazao muhimu kwa hao waliofanya kazi katika ardhi,
hupokea baraka kutoka kwa Mungu. 8 Lakini ikiwa huzaa miiba na magugu, haina tena thamani na ipo
katika hatari ya kulaaniwa. Mwisho wake ni kuteketezwa. 9 Ijapokuwa tunazungumza hivi, rafiki wapenzi,
tunashawishiwa na mambo mazuri yawahusuyo ninyi na mambo yahusuyo wokovu. 10 Kwa kuwa Mungu
si dhalimu hata asahau kazi yenu na kwa upendo mliouonesha kwa ajili ya jina lake, katika hili
mliwatumikia waamini na bado mngali mnawatumikia. 11 Na tunatamani sana kwamba kila mmoja wenu
aweze kuonesha bidii ile ile mpaka mwisho kwa uhakika wa ujasiri. 12 Hatutaki muwe wavivu, lakini
muwe wafuasi wa wale warithio ahadi kwa sababu ya imani na uvumilivu. 13 Kwa maana Mungu alipompa
Abrahamu ahadi, aliapa kwa nafsi yake, kwa kuwa asingeliapa kwa mwingine yeyote aliye mkubwa kuliko
yeye. 14 Alisema, "Hakika nitakubariki, na nitauongeza uzao wako zaidi." 15 Kwa njia hii, Abrahamu
alipokea kile alichoahidiwa baada ya kusubiria kwa uvumilivu. 16 Maana wanadamu huapa kwa yeye aliye
mkuu kuliko wao, na kwao ukomo wa mashindano yote ni kiapo kwa kuyathibitisha. 17 Wakati Mungu
alipoamua kuonesha kwa uwazi zaidi kwa warithi wa ahadi kusudi lake zuri lisilobadilika, alilithibitisha
kwa kiapo. 18 Alifanya hivyo ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu
hawezi kusema uongo, sisi tulioikimbilia hifadhi tupate kutiwa moyo kushikilia kwa nguvu tumaini
lililowekwa mbele yetu. 19 Tunao ujasiri huu kama nanga imara na ya kutegemea ya roho zetu, ujasiri
ambao unaingia sehemu ya ndani nyuma ya pazia. 20 Yesu aliingia sehemu ile kama mtangulizi wetu,
akisha kufanyika kuhani mkuu hata milele baada ya utaratibu wa Melkizedeki.

---

## Waebrania 06 Maelezo kwa jumla

### Dhana muhimu kwa sura hii

### Agano la Kiabrahamu

Katika agano Mungu alifanya na Abrahamu, Mungu aliahidi kuwafanya uzao wake kuwa taifa kubwa. Aliahidi pia kuwakinga uzao wa Abrahamu na kuwapa ardhi yao.

---

### Hebrews 6:1

**Sentensi Unganishi:**
mwandishi anendele na kile Waebrania waumini walipaswa kufanya ili wawe wakristo wakomavu. Anawakumbusha mafundisho ya msingi.

**tukiacha tulichojifunza kwanza kuhusu ujumbe wa Kristo, twapaswa kuwa na juhudi kuelekea kwenye ukomavu**
Hii inaongelea kuhusu mafundisho ya msingi kana kwamba yalikuwa ni mwanzo wa safari na mafundisho makomavu kana kwamba ni mwisho wa safari.

**tusiweke tena misingi ya toba kutoka katika kazi zisizo na uhai na imani katika Mungu,**
Mafundisho ya msingi yanaongelewa kana kwamba yalikuwa ni jengo ambalo mjenzi alianza kwa kuweka msingi. AT: "tusirudie mafundisho ya awali... ya imani katika Mungu"

**kazi zisizo na uhai**
matendo ya dhambi yanaongelwa kana kwamba yalitoka katika ulimwengu wa wafu.

**ala misingi ya mafundisho ya...hukumu ya milele**
Mafundisho ya msingi yanaongelea kana kwamba yalikuwa ni jengo ambalo mjenzi wake alianza kwa kuweka msingi. AT: "wala mafundisho ya msingi... uzima wa milele"

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

**kuwekea mikono**
Huduma hii iliwekwa kwa kumtenga mtu kwa huduma au nafasi maalum.

### Hebrews 6:4

**wale ambao waliipata nuru**
uelewa unaongelewa kana kwamba ilikuwa ni kupatiwa nuru. AT: "wale ambao awali walielewa ujumbe kuhusu Kristo"

**ambao walionja kipawa cha mbinguni**
kuonja wokovu kunaongelewa kana kwamba ni kuoonja chakula. AT: walionja nguvu ya Mungu ya kuokoa"

**kufanywa kuwa washirika wa Roho Mtakatifu,**
Roho Mtakatifu ambaye anakuja kwa waumini, anaongelewa kana kwamba ni chombo ambacho watu wangeweza kushiriki. AT: "waliopoke Roho Mtakatifu"

**ambao walionja uzuri wa neno la Mungu**
Kujifunza neno la Mungu kunaongelewa kana kwamba ilikuwa ni kuonja chakula. AT: "waliojifunza neno zuri la Mungu"

**nguvu za wakati ujao**
Hii inamaanisha nguvuza Mungu wakati ufalme wake utakapo kuwa umetimilka duniani kote. kwa mantiki hii "nguvu" ina maanishaMungu mwenyewe, ambaye anamiliki nguvu zote.

**kisha wakaanguka**
kupoteza uaminifu kwa Mungu kunaongelewa kana kwamba anguko la kimwili.AT: "walioacha kuamini katika Mungu"

**haiwezekani kuwarejesha tena katika toba**
"Haiwezekani kuwarejesha tena kwenye toba"

**wamemsulubisha Mwana wa Mungu kwa nafsi zao**
watu wanapoondoka kwa Mungu ni kana kwamba wanamsulubisha tena Yesu.

**Mwana wa Mungu**
Hiki ni cheo muhimu ambacho kinaelezea uhusiano kwa Mungu.

### Hebrews 6:7

**ardhi iliyopokea mvua inyeshayo mara kwa mara juu yake**
ardhi inufaikayo na mvua nyingi inaongelewa kana kwamba ni mtu aliyekunywa maji mengi ya mvua.

**ikatoa mazao muhimu**
Ardhi izaayo mazao inaongelewa kana kwamba iliwazalia.

**kwa hao waliofanya kazi katika ardhi**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "kwa wale kwa ajili yao mtu aliandaa ardhi"

**ardhi hupokea baraka kutoka kwa Mungu**
Mvua naa mazao vinaonekana kama ushahidi kama Mungu amemsaidia mkulima. Ardhi inaongelewa kana kwamba ni mtu ambaye angeweza kupokea baraka za Mungu.

**ipo katika hatari ya kulaaniwa**
Hii inaongelea "laana" kana kwamba ni ilikuwa ni sehemu ambayo mtu angeweza kukaribia. AT: "iko katika hatari ya Mungu kuilaani.

**Mwisho wake ni kuteketezwa**
Mungu atasababisha kila kitu katika shamba hilo kuteketea.

### Hebrews 6:9

**tunashawishiwa**
ingawa mwandishi anatumia nomino ya wingi "Tuna" mara nyingi anamaanisha yeye mwenyewe.

**ambo mazuri yawahusuyo**
Hii inamaana kuwa wanafanya vizuri kuliko wale walio mkataa Mungu, wasiomtii yeye, na hawawezi tena kutubu ili kwamba awasamene.

**mambo yahusuyo wokovu**
Nomino dhaaniwa "wokovu" inaweza kuwekwa kama kitenzi.

**Kwa kuwa Mungu si dhalimu hata asahau**
Maneno haya yanamaanisha kuwa Mungu katika haki yake atakumbuka mambo mazuri ambayo watu wake wameyafanya.

**jina lake**
"Jina" lake lina maanisha Mungu

### Hebrews 6:11

**tunatamani sana**
Ingawa mwandishi anatumia wingi lakini anamaanisha yeye mwenyewe.

**bidii**
uangalifu, kazi ngumu

**mpaka mwisho**
AT: "mpaka mwisho wa maisha yako"

**kwa ajili ya uhakika wa ujasiri**
"ili kuwa na uhakika timilifu kuwa mtapokea kile ambacho Mungu amewaahidi ninyi"

**waigaji**
"muigaji" ni mtu ambaye ana nakili tabia ya mtu mwingine.

**kuzirithi ahadi**
kupokea kile ambacho Mungu alichowaahidi waumini kinaongelewa kana kwamba ilikuwa wanarithi kitu na utajiri kutoka kwa mwanafamilia. AT: " pokea kileambacho Mungu amewaahidi"

## Hebrews 6:13

**Alisema**
Mungu akasema

**Nitakuongeza zaidi**
Neno "ongeza" hapa linasimama kwa uzao. AT: "Nitakupa uzao mwingi'

**Kile kilichoahidiwa**
Hii inaweza kusemwa katika muundo tendaji. AT: " Kile ambacho Mungu alimuahidi"

## Hebrews 6:16

**kwa warithi wa ahadi**
kwa watu ambao Mungu amewawekea ahadi wanaongelewa kana kwamba walikuwa warithi kitu na utajiri kutoka kwa mwanafamilia. AT: "kwa wote ambao wangepokea kile alichoahidi"

**kwa kusudi zuri lisilobadilika**
"kwamba kusudi lake halitabadilika kamwe" au "kwamba mara zote atafanya kile alichosema atafanya"

**kwa vitu viwili visivyobadilika**
Hii ina maana ahadi ya Mungu na kiapo cha Mungu. Wala hivi haviwezi kubadilika.

**ambavyo katika hivyo haiwezekani kabisa Mungu kudanganya**
Vikanushi hivi viwili vinaweza kumaanisha kwamba Mungu atasema kweli kuhusu hali hii. AT:"ambayo mara zote Mungu husema kweli"

**sisi, tuliokimbilia**
Waumini, ambao wanatumaini katika Mungu kwa yeye kuwalinda, wanaongelewa kana kwamba walikuwa wanakimbilia kwenye sehemu salama. AT: ""sisi, ambao tuliomtumaini yeye"

**lile lililowekwa mbele zetu**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "kile ambacho Mungu ameweka mbele zetu"

## Hebrews 6:19

**Sentensi Unganishi:**
Baada ya kumaliza onyo lake la tatu na maneno ya kuwatia moyo waumini, mwandishi wa Waebrania anaendeleza ulinganifu wake wa Yesu kama kuhani dhidi ya kuhani Melikizedeki.

**kama nanga salama na tegemewa ya roho zetu**
Kama vile nanga inanyoshikilia mtumwi kutoenda sehemu nyingine ndani ya maji, Yesu anatuweka sisi sehemu salama katika uwepo wa Mungu.

**ujasiri uingiao sehemu ya ndani nyuma ya pazia**
Ujasiri unaongelewa kana kwamba ni mtu ambaye angeweza kwenda katika mahali patakatifu pa patakatifu pa hekalu.

**sehemu ya ndani**
Hii ilikuwa ni sehemu ya ndani ya hekalu.Ilidhaniwa kuwa ndiyo sehemu Mungu alikuwa akikaa miongoni mwa watu wake. Katika sura hii sehemu hii inasimama kama mbingu na chumba cha kiti cha enzi cha Mungu.

**kama mtangulizi wetu**
Ukweli kwamba Yesu alikufa na kufufuka, na kwamba sasa yuko na Mungu Baba, inaonyesha kwamba sisi tunaoamini katika yeye tutapata mambo yaleyale.Yesu anaoglewa hapa kana kwamba ni mtu ambaye anakimbia mbele yetu na kwamba tunamfuata.

**kwa mfano wa Melikezedeki**
Hii ina maana kuwa Kristo kama kuhani ana vigezi sawa na vya kuhani Melikizedeki,

## Chapter 7

**1** Ilikuwa hivi Melkizedeki, mfalme wa Salemu, Kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Abrahamu
akirudi kutoka kuwaua wafalme na akambariki. **2** Abrahamu alimpa moja ya kumi ya kila kitu alichokuwa
amekiteka. Jina lake "Melkizedeki " maana yake" mfalme wa haki" na pia "mflame wa Salemu" ambayo ni
"mfalme wa amani." **3** Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku wala mwisho wa
maisha yake. Badala yake, anabakia kuhani milele, kama mwana wa Mungu. **4** Sasa fikiria jinsi huyu mtu
alivyokuwa mkuu. Mzazi wetu Abrahamu alimpa moja ya kumi ya vitu vizuri alivyovichukua vitani. **5** Na
hakika, ukoo wa Walawi waliopokea ofisi za kikuhani walikuwa na amri kutoka kwenye sheria kukusanya
moja ya kumi kutoka kwa watu, ambayo ni, kutoka kwa Wairaeli wenzao, pamoja na kwamba wao, pia, ni
ukoo kutoka kwa Abrahamu. **6** Lakini Melkizedeki, ambaye hakuwa wa ukoo kutoka kwa Walawi, alipokea
moja ya kumi kutoka kwa Abrahamu, na akambariki, yeye aliyekuwa na ahadi. **7** Hapo haikataliwi kwamba
mtu mdogo hubarikiwa na mkubwa. **8** Kwa jambo hili mtu apokeaye moja ya kumi atakufa siku moja,
lakini kwa jambo jingine mmoja aliyepokea moja ya kumi kwa Abrahamu ikaelezwa kama anayeishi. **9** Na
kwa namna ya kuzungumza, Lawi aliyepokea moja ya kumi, pia alilipa moja ya kumi kwa Abrahamu, **10**
kwa sababu Lawi alikuwa katika viuno vya baba yake Abrahamu wakati Melkizedeki alipokutana na
Abrahamu. **11** Sasa kama ukamilifu uliwezekana kupitia ukuhani wa Lawi, (hivyo chini yake watu hupokea
sheria), kulikuwa na hitaji gani zaidi kwa kuhani mwingine kuinuka baada ya mfumo wa Melkizedeki, na
siyo kuitwa baada ya mpangilio wa Haruni? **12** Kwa hiyo ukuhani ukibadilika, hapana budi sheria nayo
kubadilika. **13** Kwa mmoja ambaye mambo haya yalisemwa kuhusu kabila jingine, kutoka kwake hakuna
aliyehudumu madhabahuni. **14** Sasa ni wazi kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambalo Musa
hakutaja kuhusu makuhani. **15** Na haya tusemayo ni wazi hasa ikiwa kuhani mwingine atatokea kwa
mfano wa Melkizedeki. **16** Kuhani huyu mpya siyo mmoja ambaye amekuwa kuhani juu ya msingi wa
sheria zinazohusiana na uzao wa mtu, lakini katika msingi wa nguvu ya maisha yasiyoweza kuharibika. **17**
Hivyo maandiko yanashuhudia kuhusu yeye: "Wewe ni kuhani milele baada ya mfumo wa Melkizedeki." **18**
Kwa kuwa amri iliyotangulia iliwekwa pembeni kwa sababu ilikuwa dhaifu na haifai. **19** Hivyo sheria
haikufanya chochote kikamilifu. Isipokuwa, kulikuwa na ujasiri mzuri kwa hayo tunamsogelea Mungu. **20**
Na Ujasiri huu mzuri haukutokea pasipo kuzungumzia kiapo, kwa hili makuhani wengine hawakuchukua
kiapo chochote. **21** Lakini Mungu alichukua kiapo wakati aliposema kuhusu Yesu, "Bwana ameapa na
hatabadilisha mawazo yake.' wewe ni kuhani milele." **22** Kwa hili Yesu pia amekuja kuwa dhamana ya
agano bora. **23** Kwa hakika, kifo huzuia makuhani kuhudumu milele. Hii ni kwa sababu walikuwapo
makuhani wengi, mmoja baada ya mwingine. **24** Lakini kwa sababu Yesu anaishi milele, ukuhani wake
haubadiliki. **25** Kwa hiyo yeye pia anaweza kwa ukamilifu kukamilisha kuwaokoa wanaomkaribia Mungu
kupitia kwake, kwa kuwa yeye anaishi daima kwa kuomba kwa ajili yao. **26** Kwa hiyo kuhani mkuu wa
namna hii anastahili kwetu. Asiye na dhambi, hatia, msafi, aliyetengwa kutoka kwa wenye dhambi, na
amekuwa juu kuliko mbingu. **27** Yeye hakuwa na uhitaji, mfano wa makuhani wakuu, kutoa dhabihu kila
siku, kwanza kwa dhambi yake mwenyewe, na baadaye kwa dhambi za watu. Alifanya hivi mara moja kwa
wote, alipojitoa yeye mwenyewe. **28** Kwa sheria huwateua watu dhaifu kuwa makuhani wakuu, lakini neno
la kiapo, lililokuja baada ya sheria, alimteua Mwana, aliyefanywa kuwa mkamilifu milele.

---

## Waebrania 07 maelezo kwa jumla

### Muundo na Mpangilio

Watafsiri wengine wametenga kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 7:17,21, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Kuhani mkuu

Ni kuhani mkuu tu angetoa dhabihu ili Mungu asamehe dhambi na kwa hivyo lazima Yesu alikuwa kuhani Mkuu. Sheria ya Musa iliamuru kwamba kuhani mkuu atoke kwa kabila la Walawi lakini Yesu alitoka kabila la Yuda.Mungu alimfanya kuhani kama Melikizedeki aliyeishi dhabihui za Abarahamu kabla ya kuwepo kabila la Walawi.

---


generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Hebrews 7:1

**Sentensi Unganishi**
Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anaendeleza ulinganifu wake juu ya Yesu kama kuhani na kuhani Melikizedeki.

**Salem**
Hili ni jina la mji.

**Abrahamu anarudi kutoka kuwauwa wafalme**
Hii ina maanisha wakati Abrahamu na watu wake walipoenda na kuyashinda majeshi ya wafalme wanneili kumwokoa benamu yake, Lutu, na familia yake.

**ilikuwa kwake**
"Ilikuwa kwa Melikizedeki"

**mfalme wa haki... mfalme wa amani**
"mfalme wa haki... mfalme wa amani"

**Hana baba, hana mama, hana wazazi, wala mwanzo wa siku wala mwisho wa maisha yake**
Inawezekana kufikiri kutoka katika ukurasa huu kwamba Melikizedeki hakuzaliwa wala hakufa. Ingawa, ni kama inamaanisha mwandishi anamaanisha kwamba Maandiko hayaarifu chochote kuhusu wazazi wa Melkizedeki, kuzaliwa, au kifo.

## Hebrews 7:4

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anasema kwamba ukuhani wa Melikizedeki ni bora kuliko wa ukuhani wa haruni na anakumbusha kuwa ukuhani wa Haruni haukukamilisha chochote.

**huyu mtu alikuwa**
'Melikizedeki alikuwa"

**kwa upande mmoja...lakini kwa upande mwingine**
maneno haya yametumika kulinganishwa vitu viwili. Lugha yako inaweza kuwa na namna ya msisitizo kwamba mwandishi anaweka ulinganifu. Au unaweza kutumia "kwa upande mwingine"

**Wana wa Lawi ambao hupokea ukuhani**
Mwandishi anasema hili kwa sababu sio wana wote wa Lawi walikuwa makuhani.

**kutoka kwa watu**
"kutoka kwa watu wa Israeli"

**kutoka kwa ndugu zao**
Neno ndugu hapa linamaanisha kuwa wote wanahusiana kupitia kwa Abrahamu.

**wao, pia wanatoka katika mwili wa Abrahamu**
Hii ni namna nyigine ya kusema walikuwa wana wa Abrahamu.

**ambao uzao wake haukutoka kwao**
"ambao hawakuwa wana wa Lawi"

**yeye aliyekuwa na ahadi**
Mambo ambayo Mungu aliahidi kufanya kwa ajili ya Abrahamu yanaongelewa kana kwamba vilikuwa ni vitu ambavyo angeweza kumiliki.

## Hebrews 7:7

**mtu mdogo hubarikiwa na mkubwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji: AT: "Mtu wa muhimu humbariki mtu asiye wa muhimu kama yeye"

**katika jambo hili... katika jambo lile**
Maneno haya hutumika katika kulinganisha ukuhani wa Lawi na ukuhani wa Melikizedeki. Lugha yako unaweza kuwa kunaweza kuwa na namna ya kusisitiza kwamba mwandishi anafanya ulinganifu.

**imeshuhudiwa kwamba anaendelea kuishi**
haijaandikwa katika maandiko kwamba kwamba Melikizedeki anakufa. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anaandika kukosekana kwa taarifa ya kifo cha Melikizedeki kana kwamba bado anaendelea kuishi. Hii inaweza kuelezewa katika muundo tendaji. AT: "andiko linaonyesha kuwa anaendele kuishi:

**Lawi... alikuwa katika mwili wa baba yake**
kwa kuwa Lawi alikuwa hajazaliwa bado, mwandishi kana kwamba bado alikuwa katika mwili wa Abrahamu. Kwa jinsi hii mwandishi anatia hoja kuwa Lawi alilipa zaka kwa Melikizedeki kupitia Abrahamu.

## Hebrews 7:11

**sasa**
Hii haimanishi "kwa wakati huu," imetumika kuvuta usikivu kwa kipengele muhimu kinachofuata.

**kungekuwa na hitaji gani jingine zaidi la kuhani mwingine kuja kwa mfano wa Melikizedeki, na wala sio kwa mfano wa Haruni?**
Swali hili linasisitiza kwamba haikutegemewa kwamba kuhani angeweza kuja kwa mfano wa Melikizedeki.

**kuinuka**
"kuja" au "kutokeza"

**kwa mfano wa Melikizedeki**
Hii ina maana kuwa Kristo kama kuhani ana sifa zifananazo na kuhani Melikizedeki.

**na sio kutoka kwa namna ya Haruni**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "na sio kuwa kwa jinsi ya Haruni" au "ambaye ni kuhani sio kwa mfano wa Haruni"

**Kwa kuwa pindi ukuhani unapobdilishwa, sheria nayo ni lazima ibadilishwe.**
Hii inaweza kutamkwa katika mfumo tendaji. AT: " kwa kuwa Mungu alipobdilishwa ukuhani, pia alipaswa kubadlisha sheria"

### Hebrews 7:13

**Kwa ambaye**
Hii ina maanisha Yesu.

**ambaye mambo mambo haya yanasemwa kuhusu yeye**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "ambaye ninaongea kuhusu yeye

**Sasa**
Hii haimanishi "wakati huu," lakini linatumika kuvuta usikivu kwa ajili ya kipengele muhimu kinachofuata.

**Bwana wetu alizaliwa katika Yuda**
Haya maneno "Bwana wetu" linamaanisha Yesu.

**kutoka Yuda**
"kutoka katika kabila la Yuda"

### Hebrews 7:15

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii inatoka katika Zaburi ya mfalme Daudi

**haya tuyasemayo ni wazi hasa**
" tunaweza kuelewa hata zaidi." "tuna" inamaanisha mwandishi na watu anaowaandikia.

**ikiwa kuhani mwingine atatokea**
"kama kuhani mwingine atakuja"

**kwa mfano wa Melikizedeki**
Hii ina maana kwamba kristo ana sifa sawa na kuhani Melikizedeki.

**kwa msingi wa sheria zinazohusiana na uzao wa mwili**
wazo la huzao wa mtu linaongelewa kana kwamba ilikuwa inashughulika na mwili wa mtu.

**lakini katika msingi wa nguvu ya maisha yasiyo haribika**
Neno " alifanyika kuhani" linaeleweka. AT: "lakini alikuwa kuhani kwa msingi wa nguvu ya maisha ambayo hayatakoma"

**Kwa sababu maandiko yanashuhudia kuhu yeye**
Hii inaongelewa kana kwamba andiko ni mtu ambaye angeweza kushuhudia kuhusu kitu.

**kwa mfano wa Melikizedeki**
Hii ina maanisha kwamba Kristo kama kuhani ana sifa sawa na za kuhani Melikizedeki.

### Hebrews 7:18

**kulikuwa na amri ya kwanza kutanguliwa**
Mungu aliifanya amri yake ya kwanza kutofaa"

**sheria haikukamilisha chochote**
sheria inaongelewa kana kwamba alikuwa ni mtu ambaye angeweza mutenda.

**kuna utangulizi wa ujasiri mzuri**
"Mungu ametupa hoja bora ya kuwa na ujasiri"

**kuna utangulizi wa ujasiri bora iliyombele yetu ambayo kwa hiyo tunamkaribia Mungu**
Ujasiri kwa wakati ujao unaongelewa kana kwamba ni kitu ambacho kutia hicho mtu lazima amkaribie Mungu.

**tunamkaribia Mungu**
Kumwabudu Mungu na kuwa na upendeleo wake vinaongelewa kana kwamba ni tendo la kumkaribia yeye.

### Hebrews 7:20

**maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii inatoka katika Zaburiya Daudi kama mstari wa 17

**hii haikutokea pasipo kula kiapo**
Tendo la kula kiapo linaongelewa bila kusema ni nani aliyekula hicho kiapo. Japo kuwa alikuwa Mungu.

**kwa kiapo kilichotolewa kwa ambaye alimwambia**
hii inawea kusemwa katika mfumo tendaji. AT:"kwa sababu Mungu aliapa kwake kwa kusema"

### Hebrews 7:22

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anawahakikishia aumini hawa wa Kiyahudi kwamba Kristo na ukuhani ulio bora kwa sababu anaishi milele na makuhani wote waliotoka kwa Haruni walikufa.

**dhamana**
"uhakika" au "ukweli"

**kwa hakika au kwa upande mwingine**
maneno haya yametumika kulinganisha mambo mawili. Lungha yako inaweza kuwa na msisitizo kwamba mwandishi anafanya ulinganifu.

**kifo huuhuzuia kutodumu**
Hii inaweza kusemwa katika muundo tendaji. AT: '"mwishowe wanakufa na hawawezi kuendelea"

**ana ukuhani udumuo/ haubadiliki**
kazi ya kikuhani inaongelewa kana kwamba ni chombo ambach Yesu alikimiliki. AT: "yeye ni kuhani asiye badilika"

## Hebrews 7:25

**Kwa hiyo**
unaweza kufafanunua "neno "Kwa hiyo" linachomaanisha. AT: " Kwa sababu Kristo ni kuhani wetu mkuu anayeishi milele"

**wale wanaomkaribia Mungu**
"wale wanaokuja kwa Mungu kwa sababu ya kile Yesu alichofanya"

**ametukuka zaidi kuliko mbingu**
"na Mungu amemuinua juu kupita mbingu." Mwandishi anaongelea kumiliki heshima zaidi na nguvu zaidi ya mtu yeyote kana kwamba ni nafasi ambayo ni zidi ya vitu vyote. AT: "na Mungu amempaheshima na nguvu kuliko mtu yeyote"

## Hebrews 7:27

**Maelezo ya Jumla:**
Maneno "Yeye" na "mwenyewe" yanaamaniisha Kristo. Neno "yake" linamaanisha makuhani wakuu wa duniani.

**sheria uteua**
Neno sheria hapa ni neno linalosimama kwa niaba ya Mungu, ambaye alianzisha sheria. Waisraeli waliteuwa makuhani wao kwa mjibu wa sheria.

**wamaume waliokuwa dhaifu**
wanaume waliokuwa dhaifu kiroho" au "wanaume ambao ni wadhaifu kw dhambi"

**neno la kiapo, ambalo lilikuja baada ya sheria, lilimweka Mwana**
"baada ya kuwapa sheria, Mungu aliapa kwa kiapo na kumteua Mwanawe"

**kwa neno la kiapo**
neno "kiapo" limepewa nafsi na linaelezewa kana kwamba ni mtu ambaye aliongea.

**Mwana**
Hiki ni cheo muhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu.

**aliyefanywa kuwa mkamilifu**
"aliyekamilishwa kumtii Mungu na kuwa mkomavu"

## Chapter 8

[1] Sasa jambo ambalo tunasema ni hili: tunaye kuhani mkuu aliyekaa chini katika mkono wa kulia wa kiti
cha enzi Mbinguni. [2] Yeye ni mtumishi katika mahali patakatifu, hema la kweli ambalo Bwana ameliweka,
siyo mtu yeyote wa kufa. [3] Kwa maana kila kuhani mkuu huwekwa kutoa zawadi na dhabihu; kwa hiyo ni
muhimu kuwa na kitu cha kutoa. [4] Sasa kama Kristo alikuwa juu ya nchi, yeye asingekuwa kuhani zaidi ya
hapo. Kwa kuwa walikuwa tayari wale waliotoa vipawa kulingana na sheria. [5] Walihudumu kitu ambacho
kilikuwa nakala na kivuli cha vitu vya mbinguni, sawa kama Musa alipoonywa na Mungu wakati alipotaka
kujenga hema. "Ona," Mungu akasema, "kwamba tengeneza kila kitu kulingana na muundo ulioonyeshwa
juu ya mlima". [6] Lakini sasa Kristo amepokea huduma bora zaidi kwa sababu yeye pia ni mpatanishi wa
agano zuri, ambalo limekwisha kuimarishwa kwa ahadi nzuri. [7] Hivyo kama agano la kwanza lisingekuwa
na makosa, ndipo hakungekuwa na haja kutafuta agano la pili. [8] Kwa kuwa wakati Mungu alipogundua
makosa kwa watu alisema, "Tazama, siku zinakuja, 'asema Bwana, 'wakati nitakapotengeneza agano jipya
pamoja na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. [9] Halitakuwa kama agano nililofanya pamoja na baba
zao siku ambayo niliwachukua kwa mkono kuwaongoza kutoka nchi ya Misri. Kwa kuwa hawakuendelea
katika agano langu, nami sikuwajali tena,' asema Bwana. [10] Kwa kuwa hili ndilo agano nitafanya kwa
nyumba ya Israeli baada ya siku hizo,' asema Bwana. 'nitaweka sheria zangu mawazoni mwao, na
nitaziandika mioyoni mwao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. [11] Hawatafundishana kila
mmoja na jirani yake, na kila mmoja na ndugu, yake, akisema, "Mjue Bwana," hivyo wote watanijua mimi,
kutoka mdogo hadi mkubwa wao. [12] Hivyo nitaonyesha rehema kwa matendo yao yasiyo ya haki, na
sizitazikumbuka dhambi zao tena." [13] Kwa kusema "Mpya," amelifanya agano la kwanza kuwa kuukuu. Na
hilo ambalo amelitangaza kuwa kuukuu liko tayari kutoweka.

---

## Waebrania 08 Maelezo kwa jumla

### Muundo na mpangilio

Mwandishi anamalizia kwa kufafanua jinsi gani na ni kwa nini Yesu ndiye kuhani mkuu muhumu. Halafu anaanza kuzungumzia jinsi agano jipya ni bora kuliko agano Mungu alifanya na Musa.

Watafsiri wengine wametenga kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 8:8-12, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii.

### Agano jipya

Mwandishi anaelezea jinsi Yesu ameanzisha agano jipya ambalo ni bora kuliko agano Mungu alianzisha na wana wa Israeli.

---

### Hebrews 8:1

**Sentensi Unganishi:**
Baadaa ya mwandishi kuonyesha ukuhani wa Kristo ulivyo bora kuliko ukuhani wa duniani, anaonyesha kuwa ukuhani wa duniani ulikuwa ni mfano wa mambo ya mbinguni. Kristo ana huduma iliyo bora, au agano lililobora.

**Sasa**
Hii haimaanishi ni "wakati huu," lakini neno hili limetumika kuvuta usikivu kwa kipengele muhimu kinachofuata.

**tunasema**
Ingawa mwandishi anatumia wingi "tuna" kimsingi anaongea yeye mwenyewe.AT: "Ninasema" au "ninaandika"

**aliketi kwa mkono wa kuume**
Neno "mkono wa kuume" linamaanisha sehemu ya heshima. AT: "aliketi katika sehemu ya heshima"

**katika kiti cha enzi mbinguni**
Neno "Ukuu" linamaanisha Mungu, na kiti chan enzi linamaanisha utawala wa Mungu kama mtawala,

 

**hema ya kweli ambayo Bwana, sio mwanadamu, aliliweka**
watu walijenga hema za dunianikwa kutumia ngozi za wanyama zilizofungwa katika nguzo za mbao, na zikawekwa kwa namna ya hema. Hema ya kweli hapa inamaanisha hema ya mbinguni ambayo Mungu ameitengeneza.

### Hebrews 8:3

**Kwa kuwa kila kuhani mkuu huteuliwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji.AT: "kwa kuwa Mungu huteua kila kuhani'

**Sasa**
hII haimaanishi "wakati huu," lakini imetumika ili kuvuta usikivu kwenye kipengele muhimu kinachofuata.

**kwa mjibu wa sheria**
"kama Mungu anavyotaka katika sheria"

**nakala na kivuli**
Haya maneno yana kimsingi yana maana moja ili kusisitiza kwamba hema ilikuwa ni sura halisi ya hema ya mbinguni.

**kivuli cha mambo ya mbinguni**
Mwandishi anaongea hekalu la duniani, ambalo ni nakala ya hekalu la mbinguni, kana kwamba ilikuwa ni kivuli.

**Kama vile Musa alivyo onywana Mungu wakati alipokuwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. "kama vile Mungu alivyomwonya Musa wakati Musa alipokuwa"

**alipotaka kuanza kujenga hema**
Musa hakujenga hema yeye mwenyewe. Aliwaamuru watu kuijenga. AT: "alitaka kuwaawamuru watu kuijenga hema"

**"Tazama," Mungu akasema, "kwamba wewe...mlima**
unaweza kutoa nukuu. AT: "Mungu akasema, 'tazama kwamba wewe... mlima""

**tazama**
"Hakikisha"

**muundo**
"kwa muundo"

**ilioonyeshwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Ile niliyokuonyesha"

**juu ya mlima**
Mlima inanaanisha mlima Sinai.

### Hebrews 8:6

**Sentensi Unganishi:**
Sehemu hii inaanza kwa kuonyesha kwamba agano jipya ni bora kuliko agano la kale la Israeli na Yuda.

**Kristo amepokea**
"Mungu amempa Kristo"

**huduma iliyo bora zaidi. kama alivyo mpatanishi wa agano bora**
"huduma iliyo bora zaidi, kama Kristo alivyo mpatanishi wa agano bora"

**mpatanishi wa agano bora**
Hii ina maanisha kuwa Kristo alisababisha agano bora kuendelea kati ya Mungu na wanadamu.

**ambalo liko katika ahadi bora**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: ''ni agano hili ambalo Mungu alililifanya kulingana na ahadi zilizo bora" au "Mungu aliahidi vitu bora wakati alipofanya agano hili"

**Aagano la kwanza... agano la pili**
Haya maneno "kwanza" na "pili" ni namba za kawaida. AT:" agano la zamani ... agano jipya"

**halingekuwa na makosa**
"ingekuwa kamilifu"

### Hebrews 8:8

**Maelezo ya Jumla:**
Ktika nukuu hii nabii Yeremia alikuwa amesema agano jipya ambalo Mungu angefanya

**na watu**
"na watu wa Israeli"

**Angalia**
"Tazama" au "Sikiliza" au "Kuwa na tahadhari kwa lile ninalotaka kuwaambia."

**Siku zinakuja**
Ziku zijazo zinaongelewa kana kwamba zinatembea kumkabiri mzungumzaji. AT:"ktakuwa na wakati"

**nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda**
Watu wa Israeli na watu wa Yuda wanaongelewa kana kwamba wao ni nyumba. AT:"watu wa Isareli na watu wa Yuda"

**Niliwachukua kwa mkono na kuwaongoza kutoka katika ardhi ya Misri.**
Picha inawakilisha upendo mkuu wa Mungu na kujali kwake.

**hawakuendelea katika katika agano langu**
Kutii agano la Mungu kunaongelewa kana kwamba mtu alipaswa kuendelea katika hilo. AT: "hawakutii agano langu"

### Hebrews 8:10

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii inatoka kwa nabii Yeremia.

**nyumba ya Israeli**
Watu wa Israeli wanaongelewa kana kwamba walikuwa ni nyumba.

**baada ya siku hizo**
"baada ya wakati huo"

**nitaweka sheria zangu mioyoni mwao**
Sheria za Mungu zinaongelewa kana kwamba ni vyombo ambavyo vingeweza kuwekwa mahali fulani. Uwezo wa watu kufikiri kunaongelewa kana kwamba ni sehemu.AT: "Nitawawezesha kuelewa sheria zangu"

**Pia nitaziandika mioyoni mwao**
Mioyo ya watu ilifikiriwa kuwa kituo cha uaminifu kwa Mungu, na imeongelewa kana kwamba ni ukurasa ambao ungeweza kuandikwa.

**nitakuwa Mungu wao**
"Nitakuwa Mungu wanae mwabudu"

**watakuwa watu wangu**
"watakuwa watu ambao ninawajali"

### Hebrews 8:11

**Maelezo ya Jumla:**
Hii inaendeleza nukuu kutoka kwa nabii Yeremia.

**Hawatafundishana kila mmoja na jirani yake, na kila mtu na ndugu yake, akisema, 'Mjue Bwana.'**
Nukuu hii ya moja kwa moja inaweza kuengelewa kana kwamba ni nukuu isiyo ya moja kwa moja. AT: "Hawatahitaji kuwafundisha jirani zao au ndugu za kunijua"

**jirani... ndugu**
Haya maneno mawili yanalenga Waisraeli wenzao.

**Kumjua Bwana...wote watanijua mimi**
Neno "kujua" hapa linasimama kwa maana ya kutambua.

**kwa matendo yao yasiyo ya haki**
Hili linasimama kwa ajili ya watu waliofanya matendo haya yasiyo ya haki.

**Sitazikumbuka dhambi zao tena**
Neno "kumbuka" linamaanisha "sitafikiri kuhusu dhambi hizo"

### Hebrews 8:13

**liko karibu na kutowekaka**
"limekaribia kabisa kutoweka" au "litatoweka hivi karibuni"


generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Chapter 9

1 Sasa hata agano la kwanza lilikuwa na sehemu ya ibada hapa duniani na taratibu za ibada. 2 Kwani
katika hema kulikuwa na chumba kimeandaliwa, chumba cha nje, paliitwa mahali patakatifu. Katika eneo
hili palikuwa na kinara cha taa, meza na mikate ya wonyesho. 3 Na nyuma ya pazia la pili kulikuwa na
chumba kingine, paliitwa mahali patakatifu zaidi. 4 Mlikuwemo madhabahu ya dhahabu kwa kuvukizia
uvumba. Pia mlikuwemo sanduku la agano, ambalo lilikuwa limejengwa kwa dhahabu tupu. Ndani yake
kulikuwa na bakuli la dhahabu lenye manna, fimbo ya Haruni iliyoota majani, na zile mbao za mawe za
agano. 5 Juu ya sanduku la agano maumbo ya maserafi wa utukufu wafunika mabawa yao mbele ya kiti
cha upatanisho, ambacho kwa sasa hatuwezi kuelezea kwa kina. 6 Baada ya vitu hivi kuwa vimekwisha
andaliwa, Makuhani kawaida huingia chumba cha nje cha hema kutoa huduma zao. 7 Lakini kuhani mkuu
huingia kile chumba cha pili pekee mara moja kila mwaka, na pasipo kuacha kutoa dhabihu kwa ajili yake
binafsi, na kwa dhambi za watu walizozitenda pasipo kukusudia. 8 Roho Mtakatifu anashuhudia kwamba,
njia ya mahali patakatifu zaidi bado haijafunuliwa kwa vile ile hema la kwanza bado linasimama. 9 Hili ni
kielelezo cha muda huu wa sasa. Vyote zawadi na dhabihu ambavyo vinatolewa sasa haviwezi kukamilisha
dhamiri ya anayeabudu. 10 Ni vyakula na vinywaji pekee vimeunganishwa katika namna ya taratibu za
ibada ya kujiosha. Vyote hivi vilikuwa taratibu za kimwili vilivyokuwa vimeandaliwa hadi ije amri mpya
itakayowekwa mahali pake. 11 Kristo alikuja kama kuhani mkuu wa mambo mazuri ambayo yamekuja.
kupitia ukuu na ukamilifu wa hema kuu ambayo haikufanywa na mikono ya watu, ambayo si wa
ulimwengu huu ulioumbwa. 12 Ilikuwa si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe
kwamba Kristo aliingia mahali patakatifu zaidi mara moja kwa kila mmoja na kutuhakikishia ukombozi
wetu wa milele. 13 Kama kwa damu ya mbuzi na mafahari na kunyunyiziwa kwa majivu ya ndama katika
hao wasiosafi walitengwa kwa Mungu na kufanya miili yao safi, 14 Je si zaidi sana damu ya Kristo ambaye
kupitia Roho wa milele alijitoa mwenyewe bila mawaa kwa Mungu, kuosha dhamiri zetu kutoka matendo
mafu kumtumikia Mungu aliye hai? 15 Kwa sababu hiyo, Kristo ni mjumbe wa agano jipya. Hii ndiyo
sababu mauti imewaacha huru wote walio wa agano la kwanza kutoka katika hatia ya dhambi zao, ili
kwamba wote walioitwa na Mungu waweze kupokea ahadi ya urithi wao wa milele. 16 Kama kuna agano
linadumu, ni lazima kuthibitishwa kwa kifo cha mtu yule aliyelifanya. 17 Kwani agano linakuwa na nguvu
mahali kunatokea mauti, kwa sababu hakuna nguvu wakati mwenye kulifanya akiwa anaishi. 18 Hivyo
hata si lile agano la kwanza lilikuwa limewekwa pasipo damu. 19 Wakati Musa alipokuwa ametoa kila
agizo la sheria kwa watu wote, alichukua damu ya ng'ombe na mbuzi, pamoja na maji, kitambaa
chekundu, na hisopo, na kuwanyunyizia gombo lenyewe na watu wote. 20 Kisha alisema, "Hii ni damu ya
agano ambayo Mungu amewapa amri kwenu". 21 Katika hali ileile, aliinyunyiza damu juu ya hema na
vyombo vyote vilivyotumiwa kwa huduma ya ukuhani. 22 Na kulingana na sheria, karibu kila kitu
kinatakaswa kwa damu. Pasipo kumwaga damu hakuna msamaha. 23 Kwa hiyo ilikuwa lazima kwamba
nakala za vitu vya mbinguni sharti visafishwe kwa hii dhabihu ya wanyama. Hata hivyo, vitu vya mbinguni
vyenyewe vilipaswa kusafishwa kwa dhabihu iliyo bora zaidi. 24 Kwani Kristo hakuingia mahali patakatifu
sana palipofanywa na mikono, ambayo ni nakala ya kitu halisi. Badala yake aliingia mbingu yenyewe,
mahali ambapo sasa yuko mbele za uso wa Mungu kwa ajili yetu. 25 Hakuingia kule kwa ajili ya kujitoa
sadaka kwa ajili yake mara kwa mara, kama afanyavyo kuhani mkuu, ambaye huingia mahali patakatifu
zaidi mwaka baada ya mwaka pamoja na damu ya mwingine, 26 kama hiyo ilikuwa kweli, basi ingekuwa
lazima kwake kuteswa mara nyingi zaidi tangu mwanzo wa ulimwengu. Lakini sasa ni mara moja hadi
mwisho wa miaka aliyojifunua kuiondoa dhambi kwa dhabihu yake mwenyewe. 27 Kama ilivyo kwa kila
mtu kufa mara moja, na baada ya hiyo huja hukumu, 28 ndivyo hivyo Kristo naye ambaye alitolewa mara
moja kuziondoa dhambi za wengi, atatokea mara ya pili, si kwa kusudi la kushughulikia dhambi, bali kwa
ukombozi kwa wale wamgojeao kwa saburi.

---

## Waebrania 09: Maelezo kwa jumla

### Muundo na Mpangilio

Sura hii inaonyesha jinsi Yesu ni bora kuliko hekalu na sheria na masharti yake. Sura hii itakuwa ngumu kuelewa iwapo vitabo vitanu vya kwanza vya Agano la Kale havijatafsiriwa.

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

### Dhana muhimu katika sura hii

### Agano la urithi

Agano la urithi ni hati ya kisheria ambayo huelezea kile ambacho kitafanyikia mali ya mtu baada ya kifo chake.

### Damu

Katika Agano la kale, Mungu alikuwa ameamuru Waisraeli kutoa dhabihu ili dhambi zao zisamehewe. Kabla hawajatoa dhabihu hizi, walipaswa kuwaua wanyama na siyo kutoa tu miili ya wanyama hao lakini pia damu zao. Kutoa damu ni tamathali ya kumuua binadamu ama mnyama.Mungu alipeana uhai na damu yake kama dhabihu/kafara alipowaruhusu watu kumuua.Mwandishi wa Waebrania anasema kwamba hii dhabihu ni bora kuliko dhabihu ya agano la kale.

### Kurudi kwa Kristo

Yesu atarudi kumaliza kazi aliyoianzisha wakati alipokufa ili Mungu angewasamehe watu dhambi zao. Atamalizia kuwaokoa watu wanaomngojea.

### Maswala mengine ya utata katika tafsiri ya sura hii

### Agano la Kwanza

Hii inaashiria agano ambalo Mungu alifanya na Musa. Hata hivyo, kabla hajafanya agano hili, Mungu alikuwa amefanya agano na Abrahamu. Lakini hili lilikuwa ni agano la kwanza ambalo Mungu alifanya na watu wa Israeli. Unaweza amua kutafsiri "agano la kwanza" kama "agano la awali."

---

### Hebrews 9:1

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anawaweka wazi hawa waumini wa Kiyahudi kwamba sheria na hema ya agano la kale vilikuwa ni picha ya agano bora na jipya.

**Sasa**
Hii inaonyesha sehemu mpya ya fundisho.

**agano la kwanza**
Tafsiri hii kama ulivyotafsiri sura ya 8:6

**ilikuwa na taratibu**
"ilikuwa na maelekezo ya ndani" au "ilikuwa na miongozo"

**kwani**
mwandishi anaendeleza mazungumzo kutoka sura ya 8:6

**hema ilitengenezwa**
Hema ilijengwa na kuwa tayari kwa matumizi

**kinara cha taa, meza na mkate wa wonyesho**
Vyombo hivi vyote vinafuatwa neno la linaloonyesha upekee wa vyombo. Kwa sababu mwandishi anadhani kwamba wasomaji wake tayari wanafahamu kuhusu vitu vyombo hivi.

**mkate wa wonyesho**
mkate wa wonyesho mbele za Mungu au mkate ambao makuhani waliuwakilisha kwa Mungu.

### Hebrews 9:3

**nyuma ya pazia la pili**
pazia la kwanza kulikuwa na ukuta wa nje wa hema, hivyo pazia la pili lilikuwa ni pazia la pili kati ya mahali patakatifu na mahali patakatifu pa patakatifu.

**pili**
Hii ni nambaya kawaida ya namba mbili

**ndani yake**
"Ndani ya sanduku la agano"

**Fimbo ya Haruni iliyoota maua**
Hii ina maanisha wakati Mungu alipoonyesha kwa watu wa Israeli kwamba alikuwa amemchagua Haruni kama kuhani kwa kuichipusha maua fimbo ya Haruni.

**kuchipua**
"kuwa na maua" au "kuchipua" au "ilikuwa na kuendelea"

**mbao za agano**
"Mbao" ni vipande bapa vya mawe vilivyokuwa na maandishi juu yake. Hizi zinamaanisha mbao za mawe ambazo ziliandkwa amri kumi.

**makerubi walifunika juu**
wakati Waisraeli walipokuwa wakitengeneza sanduku la agano, Mungu aliwaamuru Waisraeli kuchonga makerubi wawili wanatazamana pamoja

na mbao zao zigusa juu ya kifuniko upatanisho cha sanduku la agano. Hapa vinaongelewa kana kwamba kama vinaweka kivuri kwenye sanduku la agano.

**ambao hatuwezi**
Ingawa mwandishi anatumia kiwakilishi cha wingi "tuna" kimsingi anasema kwa nafsi yake mwenyewe.

### Hebrews 9:6

**Baada ya vitu hivi kuandaliwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji.AT: "Baada ya makuhani kuandaa vitu hivi"

**na sio pasipo damu**
Hii inaweza kusemwa katika muundo tendewa. AT: "na mara zote alileta damu"

**damu**
Hii ni damu ya dume na mbuzi ambazo kuhani mkuu alipaswa kudhabihu siku ya upatanisho.

### Hebrews 9:8

**njia ya kuingia mahali patakatifu zaidi ilikuwa haijafunuliwa bado**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mungu alikuwa bado hajaifunua njia ya sehemu takatifu zaidi"

**mahali patakatifu zaidi**
Maana zinazowezekana: 1) chumba cha ndani cha hema duniani au 2) Uwepo wa Mungu mbinguni.

**hema la kwanza bado lilikuwa limesimama**
Maana zinazowezekana: 1) "chumba cha nje cha hema bado kinasimama" au 2) "hema ya duniani na taratibu za dhabihu zilikuwa zikiendelea."

**kielelezo**
"Hii ilikuwa ni "picha" au "Hii ilikuwa ni alama"

**kwa muda uliopo**
"kwa sasa"

**ambayo kwa sasa yanatolewa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. "ambayo sasa makuhani wanatoa"

**haviwezi kukamilisha dhamiri ya anayeabudu/ mwabudu**
Mwandishi anaongelea dhamiri ya mtu kana kwamba ni kilikuwa ni chombo ambacho kilikuwa kikifanywa bora zaidi. Dhamiri ya mtu ni ni ujuzi wa kujua baya na jema. Pia ni uelewa wake kama amekosa au amefanya jema. Na kama akifahamu kwamba ametenda baya tunasema anajisikia hatia.

**taratibu kwa ajili ya mwili**
Mwili hapa unamaanisha mwili wa binadamu." AT: "taratibu za mwili"

**taratibu za kimwili**
"desturi za maisha ya kimwili"

**Hizi zilikuwa desturi za kimwili ambazo zilizotolewa**
"Mungu aliandaa taratibu zote hizi kwa ajili ya mwili"

**ambazo zilizotolewa hadi mpangilio mpya ungeweza kuumbwa**
Hii inawezakusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Kwamba Mungu alitoa hadi alipoumba mpangilio mpya"

**Mpangilio mpya**
"agano jipya"

### Hebrews 9:11

**Sentensi Unganishi:**
Baada ya kufafanua huduma ya hema la agano chini ya sheria ya Mungu, mwandishi anaweka bayana kwamba huduma ya Kristo chini ya agano jipya ni bora pia kwa sababu imefunikwa kwa damu yake. Ni bora pia kwa sababu Kristo ameingia hekalu la kweli, ambalo ni uwepo wa Mungu mbinguni, badala ya ya kuingia, kama makuhani wakuu, ndani ya hema ya duniani, ambayo kimsingi ilikuwa ni nakala isiyo timilifu.

**Vitu vizuri**
Hii haimaanishi vitu vinavyoshikika. Inamaanishavitu vizuri ambavyo Mungu ameahidi katika agano lake jipya.

**hema kuu na ukamilifu zaidi**
Hii inamaanisha hema la mbingunini muhimu zaidi na timilifu zaidi ya hema ya duniani.

**ambayo haikufanywa kwa mikono ya binadamu**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "ambayo haikufanywa kwa mikono ya binadamu"

**mikono ya binadamu**
"Mikono" inamanisha mtu.

**mahali patakatifu zaidi**
Uwepo wa Mungumbinguni unaongelewa kana kwamba kana kwamba ilikuwa sehemu takatifu zaidi, chumbacha ndani cha hekalu.

### Hebrews 9:13

**kunyunyiziwa kwa majivu kwa hao ambao hawajatakaswa**
Kuhani angemimina kiasi kidogo cha majivu kwa watu wasiosafi.

**je si sana zaidi damu ya Yesu...kuosha nafsi zetu kutoka katika matendo mafu ili kumtumikia Mungu aliye hai?**
Mwandishi anatumia nukuu kusisitiza kwamba dhabihu ya Kristo ilikuwa na nguvu. AT: Hivyo hakika damu ya Kristo itatusafisha nafsi zetu hata zaidi kutoka katika kazi/ matendo mafu na kumtumikia Mungu aliye hai! Kwa sababu, kupitia

kwa kupitia Roho wa milele, alijitoa mwenyewe pasipo hatia kwa Mungu.

**damu ya Kristo**
"damu" ya Yesu inasimama kwa kifo chake.

**kusafisha dhamiri zetu**
"Dhamiri" hapa inamaanisha mtu kujisikia hatia. Kwa sababu Yesu alijidhabihu yeye mwenyewe, waumini hawapaswi tena kujisikia hatia kwa ajili ya dhambi zao walizozifanya kwa sababu amewasamehe.

**waa**
Hii ni dhambi ndogo au kosa la kimaadili hapa linaongelewa kana kwamba lilikuwa dogo,doa lisilo la kawaida kuharibu juu ya mwili wa Kristo.

**safisha**
"kusafisha" linasimama kwa tendo la nafsi zetu kupokea msamaha wa kutokuwa na hatia kwa ajili ya dhambi tulizozitenda

**hao walioitwa na Mungu**
wale ambao Mungu amewateua au kuchaguliwa na kuwa watoto wake

**Kazi/ matendo mafu**
matendo mafu yanaongelewa kana kwamba yalikuwa yakitoka katika ulimwengu wa wafu.

**Kwa sababu hii**
"kama matokeo" au "kwa sababu hii"

**Ni mjumbe/ mpatanishi wa agano jipya**
Hii inamaanisha Kristo alisababisha agano jipya kati ya Mungu na wanadamu kuwepo.

**agano la kwanza**
tafsiri hii kama ulivyotafsiri 8:6

**wale walioitwa**
Hii inaweza kuelezwa katika mfumo tendaji. AT: "wale ambao Mungu aliowachagua kuwa wana wake"

**urithi**
upokeaji wa kile ambacho Mungu alikuwa amewaahidi waumini kunaongelewa kana kwamba ilikuwa ni kurithi kitu na mali kutoka katika mwanafamilia.

### Hebrews 9:16

**wosia**
hati ya kisheria ambayo inamtaja mtu ambaye angepokea zile mali wakati mwenye mali akifa.

**kifo cha mtu aliyetenda ni lazima kihakikishwe**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "mtu ni lazima ahakikishe kwamba mtu aliweka wosia amekufa"

### Hebrews 9:18

**hivyo hata agano la kwanza halikuanzishwa pasipo damu**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Hivyo Mungu alianzisha hata lile agano la kwanza kwa damu"

**agano la kwanza**
Tafsiri hii kama ulivyotafsiri 8:6

**damu**
kifo cha wanyama waliotolewa dhabihu kunaongelewa kana kwamba hakukuwa na kitu kingine isipokuwa damu.

**alichukua damu... pamojas na maji...na kunyunyiza...gombo... na watu wote**
Kuhani alichovyawa hissopo katika damu na maji na kisha alikitikisa kijiti cha hissopo na kudondosha damu na maji juu ya magombo na watu.Kunyunyiza damu lilikuwa ni tendo la ishara lililofanywa na makuhani ambalo kwa hilo walipata faida ya agano kwa watu na vyombo. Na hapa upokelewaji wa gombo na watu vinafanywa upya.

**hisoppo**
mmea uliotumika katika ibada ya kunyunyiza

**damu ya agano**
"Damu" hapa linamaanisha kifo cha wanyama waliotolewa dhabihu ili kuftimiza matakwa ya agano.

### Hebrews 9:21

**alinyunyuzia**
"Musa alinyunyuzia"

**nyunyuzia**
Kunyunyuzia kulikuwa ni tendo la ishara ambalo lilifanywa na makuhani ambalo kwa hilo walipata faida ya agano kwa watu na kwa viyombo.

**Vyombo vyote vilivyotumiwa katika huduma**
huu ni mkebe au chombo ambacho unaweza kubeba vyombo. Hii inamaanisha vyombo au kitu. AT: " vyombo vyote vilivyotumika katika huduma"

**vilitumika katika huduma**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Makuhani walivitumia katika kazi zao"

**karibia kila kitu kinatakaswa kwa damu**
kufanya kitu kipokelewe na Mungu kunafanywa kana kwamba kitu hicho kilikuwa kinatakaswa. Wazo hili linaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Makuhani hutumia damu kusafisha karibia ila kitu"

**damu**
Hapa damu ya mnyama inaongelewa kuhusu kifo cha mnyama.

**Hakuna msamaha wa dhambi pasipo kuwagika damu**
Hapa "kumwaga damu" kunamaanisha kwa kitu kufa kama dhabihu kwa Mungu. mambo haya hasi yanaweza kumaanisha msamaha wote unapatikana kwa njia ya kumwaga damu.

**msamaha**
"msamaha wa dahmbi ya watu"

### Hebrews 9:23

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anasisitiza kwamba Kristo (sasa yuko mbinguni anatuombea) alipaswa kufa mara moja tu kwa ajili ya dhambi na kwamba atarudi duniani mara ya pili.

**nakala ya vitu vya mbinguni vinapaswa kusafishwa kwa dhabihu ya hawa wanyama**
"Makuhani wanapaswa kutumia dhabihu hii ya wanyama kusafisha nakala za vitu vya mbinguni"

**vitu vya mbinguni vyenyewe vilipaswa visafishwe kwa dhabihu zilizo bora zaidi**
Ile ni bora zaidi ya dahabihu zilizotumika kusafisha nakala za duniani. Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "kama kwa vitu vya mbinguni vyenyewe, Mungu alipaswa kuvisafisha kwa dhabihu iliyo bora"

**ilitengenezwa kwa mikono**
"Mikono" hapa inamaanisha mwanadamu. AT: "ambayo wanadamu walitengeneza na"

**ya kitu halisi**
"sehemu ya kweli na takatifu ya patakatifu pa patakatifu"

### Hebrews 9:25

**Hakuingia kule**
" Hakuingia mbinguni"

**mwaka baada ya mwaka**
"kila mwaka" au "mwaka baada ya mwa

**na damu ya mwingine**
Hii inamaanisha na damu ya mnyama wa kafara, na sio kwa damu yake mwenyewe.

**na kama hiyo ilikuwa kweli/ sababu**
"Kama alipaswa kutoa mara nyingi"

**tangu mwanzo wa ulimwengu**
Uumbaji wa dunia unaongelewa kana kwamba ni jengo na msingi wake ulikuwa sehemu ya kwanza kujengwa. AT: "tangu Mungu alipoanza kuiumba dunia"

**amefunuliwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Mung amemfunua"

**kuindoa dhambi kwa dhabihu yake mwenyewe**
Hii inaongea kuhusu dhambi kana kwamba kilikuwa ni chombo ambach mtu angeweza kukiondoa. AT: "kumsababisha Mungu kusamehe dhambi kwa kujidhabihu mwenyewe"

### Hebrews 9:27

**Pia Kristo, ambaye alitolewa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "Pia Kristo, ambaye "aliyejitoa mwenyewe"

**kuziondoa dhambi**
Tendo la kutufanya wasio na hatia badala ya kuwa na hatia kwa ajili ya dhambi zetu kunaongelewa kana kwamba dhambi zetu zilikuwa vyombo ambavyo vinashikika ambavyo Kristo aliweza kuzibeba.

**dhambi**
dhambi inamaanishahatia ambayo watu waliyonayo mbele za Mungukwa sababu ya dhambi walizotenda.

---

## Chapter 10

1 Kwa vile sheria ni kivuli cha mambo mema yajayo, si yale yaliyo halisi. Sheria kamwe haiwezi
kuwakamilisha wale ambao wanaomkaribia Mungu kwa njia ya dhabihu zilezile ambazo makuhani
waliendelea kutoa mwaka baada ya mwaka. 2 Au vinginevyo dhabihu hizo zisingeweza kukoma kutolewa?
Kwa kigezo hicho waabuduo, wakiwa wamesafishwa mara moja, wasingelikuwa na utambuzi zaidi wa
dhambi. 3 Bali katika dhabihu hizo kuna ukumbusho wa dhambi zilizotendwa mwaka baada ya mwaka. 4
Kwa kuwa haiwezekani kwa damu ya mafahari na mbuzi kuziondoa dhambi. 5 Wakati Kristo alipokuja
duniani, alisema, "Hamkutamani matoleo au dhabihu, badala yake, mliandaa mwili kwa ajili yangu. 6
Hamkuwa na thamani katika matoleo yote ya kuteketezwa au dhabihu kwa ajili ya dhambi. 7 Kisha
nilisema, "Ona, hapa ninayafanya mapenzi yako, Mungu, kama ilivyoandikwa kunihusu mimi katika
gombo". 8 Alisema kama ilivyo semwa hapo juu: "Hamkutamani dhabihu, matoleo, au sadaka ya
kuteketezwa kwa ajili ya dhambi, wala hukuona furaha ndani yake" dhabihu ambazo zinatolewa kulingana
na sheria. 9 Kisha alisema, "Ona, niko hapa kufanya mapenzi yako". Ameweka pembeni taratibu zilizo za
awali ili kuimarisha zile za pili. 10 Katika taratibu za pili, tumekwisha tengwa kwa Mungu kwa mapenzi
yake kupitia kujitoa kwa mwili wa Yesu Kristo mara moja kwa nyakati zote. 11 Ni kweli, kila kuhani
husimama kwa huduma siku kwa siku, akitoa dhabihu ile ile, ambayo, kwa vyovyote, kamwe isingeweza
kuziondoa dhambi. 12 Lakini baada ya Kristo kutoa dhabihu mara moja kwa dhambi milele yote, aliketi
mkono wa kuume wa Mungu, 13 akisubiri mpaka maadui zake watiwe chini na kufanywa kiti kwa ajili ya
miguu yake. 14 Kwa kuwa kwa njia ya toleo moja amewakamilisha milele wale ambao wametengwa kwa
Mungu. 15 Na Roho Mtakatifu pia ashuhudia kwetu. Kwa kuwa kwanza alisema, 16 "Hili ni agano
nitakalofanya pamoja nao baada ya siku hizo; asema Bwana: nitaweka sheria zangu ndani ya mioyo yao,
na nitaziandika katika akili zao". 17 Kisha alisema, "Hawatazikumbuka tena dhambi na matendo yao
mafu". 18 Sasa mahali palipo na msamaha kwa hawa, hakuna tena dhabihu yoyote kwa ajili ya dhambi. 19
Kwa hiyo, ndugu, tunao ujasiri wa kuingia mahali patakatifu zaidi kwa damu ya Yesu. 20 Hiyo ni njia
ambayo ameifungua kwa ajili yetu kwa njia ya mwili wake, mpya na hai inayopitia kwenye pazia. 21 Na
kwa sababu tunaye kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu, 22 na tumkaribie na moyo wa kweli katika
utimilifu wa uhakika wa imani tukiwa na mioyo iliyonyunyiziwa safi kutoka uovu wa dhamiri na kuwa na
miili yetu iliyooshwa kwa maji safi. 23 Basi na tushikilie kwa uthabiti katika ungamo la ujasiri wa tumaini
letu, bila ya kugeuka, kwa sababu Mungu aliyeahidi ni mwaminifu. 24 Na tuzidi kutafakari namna ya
kumtia moyo kila mmoja kupenda na matendo mema. 25 Na tusiache kukusanyika pamoja, kama
wafanyavyo wengine. Badala yake, kutiana moyo kila mmoja zaidi na zaidi, kama muonavyo siku
inakaribia. 26 Kama tukifanya makusudi kuendelea kutenda dhambi baada ya kuwa tumepokea elimu ya
ukweli, Dhabihu nyingine ya dhambi haisalii tena. 27 Badala yake, kuna tarajio pekee la hukumu ya
kutisha, na ukali wa moto ambao utawateketeza maadui wa Mungu. 28 Yeyote ambaye ameikataa sheria
ya Musa hufa bila rehema mbele ya ushuhuda wa mashahidi wawili au watatu. 29 kiwango gani zaidi cha
adhabu unafikiri kinamstahiri kilammoja ambaye amemdharau mwana wa Mungu, yeyote aliyeitendea
damu ya agano kama kitu kisicho kitakatifu, damu ambayo kwayo aliiweka wakfu kwa Mungu - yeyote
ambaye amemtukana Roho wa neema? 30 Kwakuwa tunajua mmoja ambaye aliyesema, "Kisasi ni changu,
nitalipa". Na tena, "Bwana atawahukumu watu wake". 31 Ni jambo la kuogofya mtu kuangukia katika
mikono ya Mungu aliye hai! 32 Lakini kumbuka siku zilizopita, baada ya kutiwa kwenu nuru, ni jinsi gani
mliweza kuvumilia maumivu makali. 33 Mlikuwa mmewekwa wazi katika dhihaka ya matukano na mateso,
na mlikuwa washiriki pamoja na wale waliopitia mateso kama hayo. 34 Kwa kuwa mlikuwa na moyo wa
huruma kwa hao waliokuwa wafungwa, na mlipokea kwa furaha adhabu ya urithi wenu, mkijua kwamba
ninyi wenyewe mlikuwa na urithi bora na wa kudumu milele. 35 Kwa hiyo msiutupe ujasiri wenu, ulio na
zawadi kuu. 36 Kwa kuwa mnahitaji uvumilivu, ili kwamba mpate kupokea ambacho Mungu amekiahidi,
baada ya kuwa mmekwisha yatenda mapenzi yake. 37 Kwa kuwa baada ya kitambo kidogo, mmoja
anayekuja, atakuja hakika na hatakawia. 38 Mwenye haki wangu ataishi kwa imani. Kama atarudi nyuma,
sitapendezwa naye." 39 Lakini sisi si kama wale warudio nyuma kwa kuangamia. Badala yake, sisi ni
baadhi ya wale tulio na imani ya kuzilinda roho zetu.

---

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Waebrania 10 Maelezo kwa jumla.

### Muundo na mpangilio

Katika hii sura, mwandishi anamalizia kwa kufafanua jinsi sadaka ya Yesu ni bora kuliko sadaka zilizotolewa hekaluni.

Watafsiri wengine wametenga kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 10:5-7,:15-17, 37-38, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Hukumu ya Mungu na tuzo

Kuishi kitakatifu ni muhimu kwa Wakristo. Mungu atawajibisha watu jinsi walivyoishi maisha yao ya Kikristo. Ingawa hakutakuwa na hukumu ya milele kwa Wakristo, matendo yasiyo pendeza Mungu yatakuwa na matokeo. Zaidi ya hayo maisha ya uaminifu yatatuzwa. , and and )

### Maswala mengine ya utata katika tafsiri ya sura hii.

### Maana damu ya fahali na mbuzi haiwezi kamwe kuondoa dhambi" (Waebrania 10:4)

Dhabihu zenyewe hazikuwa na nguvu za kuokoa. Zilifanikiwa kwa sababu zilikuwa dhihirisho la imani ambayo ilitokana na aliyekuwa anatoa hiyo Dhabihu. ilikuwa ni sadaka ya Yesu inayofanya sadaka hizi "kuondoa dhambi". Kulingana na hayo, Mungu hataki sadaka iltolewao bila imani. and )

### "Agano nitakalofanya"

Haiko wazi iwapo huu unabii ulikuwa unatimizwa wakati mwandishi huyu alikuwa anaandika ama iwapo ungetimizwa baadaye. Mtafsiri aepuke kusema wakati muda wa agano hili inaanza. and )

---

### Hebrews 10:1

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anaonyesha udhaifu wa sheria na dhabihu zake, kwa nini Mungu aliwapa sheria, na utimilifu wa ukuhani mpya na dhabihu ya Kristo.

**sheria ni kivuli cha mambo mema yajayo**
Hii inaongewa kuhusu sheria kana kwamba kilikuwa ni kivuli. Mwandishi anaongea kwamba sheria haikuwa vitu vizuri ambavyo Mungu alikuwa ameviahidi. Ni sehemu ndogo tu ya mambo mazuri ambayo Mungu alipaswa kuyafanya.

**si yale yaliyo halisi ya yale mambo yenyewe**
" sio vitu halisi vyenyewe"

**mwaka hadi mwaka**
"kila mwaka"

**dhabihu hizo zisingeweza kukoma kutolewa**
Mwandishi antaumia swali kuelezea kwamba dhabihu zilikuwa na nguvu ya ukomo. "wangekuwa wameacha kudhabihu dhabihu"

**ilikoma**
"sitisha"

**Kwa sababu hiyo**
"kwa hali hiyo"

**wakiwa wamesafishwa**
Dhambi za watu zinaongelewa kana kwamba ziklikuwa zikioshwa ana kwa ana. AT: " Kama Mungu alikuwa tayari amekwisha samehewa dhambi zao"

**wasingekuwa na utambuzi**
"wangeweza kufahamu kuwa hawana hatia ya dhambi tena."

**haiwezekani kwa damu mafahari na mbuzi kuziondoa dhambi**
Dhambi zinaongelewa kana kwamba zikuwa vyombo ambavyo damu ya wanyama ingeweza kuziondoa. AT: "Kwa sababu haiwezekani kabisa Mungu kusamehe dhambi kwa kwa sababu ya damu ya mafahar na mbuzi.

**damu ya mafahari na mbuzi**
"Damu" hapa inamaanisha kwa wanyama hawa waliokuwa wanakufa kwa kama dhabihu kwa Mungu.

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

### Hebrews 10:5

**Maelezo ya Jumla:**
Maneno ya Kristo alipokuwa duniani yalikuwa yamesemwa katika nukuu hii kutoka Zaburi ya Daudi.

**ambayo ulitamani**
"Wewe" hapa ni nafsi ya umoja na inamaanisha Mungu.

**mliandaa**
"kufanya tayari"

**kisha nilisema**
"Nilisema" inamaanisha Kristo

**kama ilivyoandikwa katika gombo kuhusu mimi**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: " kama manabii walivyoandika katika gombo kuhusu mimi"

**gombo**
Hii inamaanisha maandiko au maandiko matakatifu.

### Hebrews 10:8

**Maelezo ya Jumla:**
pamoja na kwamba anabadilisha maneno polepole, mwandishi anarudia nukuu hii kufoka Zaburi ya Daudi kusisitiza.

**dhabihu...sadaka...au sadaka za kuteketezwa... dhabihu kwa ajili ya dhambi**
Tafsiri maneno haya kama ulivyotafsiri 10:5

**amabyo hutolewa**
"ambayo makuhani hutoa"

**Ona/tazama**
"Tazama" au "sikiliza"

**ameweka pembeni taratibu za awali**
Jina la tendo dhaaniwa "taratibu"/ tendo hapa inamaanisha njia ya kudhabihu kwa ajili ya dhambi.Kusitisha kufanya kunaongelewa kana kwamba kilikuwa ni chombo ambacho kingeweza kuondolewa.

**taratibu za awali... taratibu za pili**
Maneno "kwanza" na "pili" ni namba za kawaida.AT: "taratibu za zamani ...taratibu mpya"

**ili kuanzishe utaratibu wa pili**
Kuanzisha njia ya pili ya kudhabihu inaongelewa kana kwamba kuanzisha utaratibu AT: "ill kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi kwa mara nyingine"

**Tumetakaswa/ tumetengwa**
"Mungu ametutakasa" au "Mungu ametuweka kwake kwa ajili yake"

**tumekwisha kutengwa kwa Mungu kwa mapenzi yake**
"Mungu alitaka Kristo kujitoa mwenyewe dhabihu na kwamba dhabihu ilishatutenga sisi kwa Mungu"

**kupitia dhabihu ya mwili wa Yesu Kristo**
"wakati Yesu Kristo alipotoa mwili wake kama dhambihu" au "kwa sababu Yesu Kristo aliudhabihu mwili wake"

### Hebrews 10:11

**kwa upande mwingine ... na kwa upande mwingine**
Haya maneno yanatumika kulinganisha vitu viwili . Lugha yako inaweza kuwa na njia ya kusisitiza kwamba mwandishi anaweka ulinganifu. Au unaweza kutumia "Lakini."

**siku kwa siku**
"siku hadi siku" au "kila siku"

**haiwezi kuziondoa dhambi**
Hii inaongelea. dhambi kana kwamba ni chombo ambacho mtu anaweza kukiondoa. AT: "haiwezi kumfanya Mungu asamehe dhambi"

**hadi maandui zake wamewkwa chini ya miguu yake**
kuteswa kwa maadui wa Kristo kunaongelewa kana kwamba ni sehemu iliyotengenezwa kwa ajili yake kupumzishia migu yake. AT: "hadi Mungu atakapowaseta maadui wa Kristo na kuwa kana kiti cha miguu yake"

**wale ambao wametengwa kwa Mungu**
"wale ambao Mungu amewatenga kwa ajili yake mwenyewe"

### Hebrews 10:15

**Maelezo ya Jumla:**
Hii ni nukuu kutoka kwa nabii Yeremia katika Agano la Kale.

**pamoja nao**
"amoja na watu wangu"

**baada ya siku hizo**
"wakati wa agano la kwanza na watu wangu ulipokwisha"

**Nitaziweka sheria zangu ndani ya mioyo yao, na nitaziandika katika akili zao**
Mioyo ya watu na akili vinaongelewa kana kwamba sheria ya Mungu ingeweza kuwekwa au kuandikwa juu yake. AT: "Nitawasababisha kuzielewa shria zangu na nitawasababisha kuzitii sheria zangu"

### Hebrews 10:17

**Maelezo ya Jumla:**
Hii inaendeleza nukuu ya nabii Yeremia katika Agano la Kale

**Sitazikumbuka dhambi zao na makosa yao**
Hii ni sehemu ya pili ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu (tazama 10:15). Kisha asema, "Sitazikumbuka dhambi zao na makosa yao."

**Sitazikumbuka dhambi zao**
"Sitazikumbuka dhambi zao"au "sitafikiri tena kuhusu dhambi zao"

**Sasa**
Hii haimaanishi "wakati huu," lakini imetumika kuvuta usikivu kwa kipengele kinachofuata.

**mahali palipo na msamaha kwa mambo haya**
"wakati Mungu aliposamehe mambo haya"

**hakuna tena dhabihu yeyote kwa ajili ya dhambi**
"watu wao hawahitajiki kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi"

## Hebrews 10:19

**Sentensi Unganishi:**
Baada ya kuweka wazi kwamba kuna dhabihu moja kwa ajili ya dhambi, mwandishi anaendelea na picha ya patakatifu pa patakatifu katika hekalu, mahali ambapo kuhani mkuu aliweza kuingia kila mwaka na damu ya dhabihu

**Ndugu**
Hii inamaanisha kwa waumini wote katika Kristo awe mwanaume au mwanamke. "dada" au "waumini"

**mahali patakatifu zaidi**
Hii inamaanisha uwepo wa Mungu, sio mahali patakatifu zaidi katika hema ya zamani.

**kwa damu ya Yesu**
"Damu ya Yesu" inamanisha kwa kifo cha Yesu.

**njia iliyo hai**
pengine inamaana 1) Njia hii mpya kwa Mungu kwamba Yesu ametoa matokeo ndani ya waumini kuishi milele au 2) Yesu yu hai, na na ni njia ambayo waumini wanaingia kuingia katika uwepo wa Mungu.

**kwa jinsi ya mwili wake**
neno mwili hapa inasimama kama kwa mwili wa Yesu, na mwili wake unasimama kwa kifo chake the kujidhabihu. AT: "kwa jinsi ya mwili wake"

**Tunaye kuhani Mkuu juu ya nyumba ya Mungu**
Hii ni lazima itafsiriwe katika namna kuweka wazi kwamba Yesu ni "kuhani Mkuu."

**juu ya nyumba**
"Msimamizi wa nyumba"

**nyumba ya Mungu**
"watu wote wa Mungu"

**Tumkaribie**
Kumkaribia hapa inasimama kwa kumwabudu Mungu, kama kuhani alipaswa kwenda juu ya mimbali ili kudhabihu wanyama kwa Mungu.

**mioyo imenyunyiziwa safi**
"mioyo ambayo Mungu ameinyunyizia kwa damu ya Yesu na kuifanya safi"

**mioyo yetu ikiwa imenyunyizwa na kutakaswa**
"kana kwamba alifanya mioyo yetu safi kwa damu yake"

**kunyunyiziwa**
"kazi ya kuweka vitu kuwa safi"

**baada ya mikono yetu kuwa imeoshwa kwa maji maji halisi**
"kana kwamba alikuwa ameosha miili yetu kwa maji halisi"

**miili yetu imeoshwa kwa maji halisi**
Kama mtafasirianaelewa kwamba sentensi hii yanamaanishaubatizo wa Kikristo, hivyo maji ni maji halisi na sio mfano. Lakini kama maji yanachukuliwa kama maji, hivyo "halisi" inasimama kwa niaba ya usafi wa kiroho ambao ubatizo unaosemwa hapa umetimiliza. "Kuoshwa" kunasimama kama waumini kuwa kupokelewa na Mungu.

## Hebrews 10:23

**shikilia kwa udhabiti ungamo la tarajio la ujasiri wetu**
"endelea kuwaambia watu kwamba tuna ujasiri kwa sababu tunaamini kuwa Mungu atatenda kile alichoahidi kutenda"

**pasipo kugeukageuka/ kuyumba yumba.**
pasipokuwa na kuwa na hakika" au "pasipokuwa na shaka"

**Tusiache kukusanyika pamoja**
"tusiache kujumuika pamoja kwa ajili ya ibada"

**kadri mwonavyo siku inakaribia**
"Kama mnavyofahamu kuwa Kristo atakuja hivi karibuni"

## Hebrews 10:26

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anatoa onyo la nne.

**kwa makusudi**
"kwa kukusudia"

**baada ya kuwa tumepokea ujuzi wa kweli**
Ujuzi wa kweli kunaongelewa kana kwamba ni chombo ambacho kinaweza kumpa mtu mmoja hadi mwingine. AT: "baaba ya kuwa tumejifunza kweli"

**dhabihu ya dhambi haipo tena**
"hakuna awezaye kutoa dhabihu ambayo Mungu atatusamehe dhambi zetu"

**kweli**
Ukweli kuhusu Mungu.

**hakuna tena dhabihu kwa ajili ya dhambi**
Hakuna mtu yeyote awezaye kutoa dhabihu mpya kwa sababu dhabihu ya Kristo ndiyo pekee inayofanya kazi.

**dhabihu kwa ajili ya dhambi**
"dhabihu kwa ajili ya dhambi" inasimama kama njia tendaji ya kudhabihu wanyama ili kuondoa dhambi"

**ya hukumu**
ya hukumu ya Mungu. ambayo, Mungu atahukumu.

**ukali wa moto ambao utawateketeza adui wa Mungu**
Ukali wa Mungu unaongelwa kana ni moto ambao ungechoma maadui wake.

## Hebrews 10:28

**wawili au watatu**
Imepewa maana ya kwambahii inamaanisha "angalau wawili au watatu"

**kiwango gani zaidi cha adhabu unafikiri kinamstahili...neema?**
Mwandishi anasisitiza ukuu wa adhabu kwa wale wote wanaomkataa Kristo.

**amemdharau mwana wa Mungu**
Kutokumjali Kristo na kumtukana kunaongelewa kana kwamba mtu anakanyaga.

**ambaye ameihesabu damu ya agano kama sio takatifu**
Hii inaonyesha jinsi mtu alivyokanyaga Mwana wa Mungu. Kwa kuihesbu damu ya agano kama sio takatifu"

**Mwana wa Mungu**
Hili ni jina muhimu la cheo cha Yesu

**damu ya agano**
"damu" hapa inasimama kama kifo cha Kristo, ambacho kwa hicho Mungu alianzisha agano jipya.

**damu ambayo kwa hiyo alitakaswa**
"damu ambayo Mungu alimtakasa kwa hiyo"

**Roho wa neema**
"Roho wa Mungu anayetoa neema"

## Hebrews 10:30

**Maelezo ya Jumla:**
Neno "tuna" linamaanisha kwa mwandishi na waumini wote. Nukuu hizi mbili zinatoka kwenye sheria ambayo Musa alitoa katika Agano la Kale.

**kisasi ni juu yangu**
kisasi kinaongelewa kana kwambani chombo ambacho kinatoka kwa Mungu, ambaye alikuwa na haki ya kufanya na kama alivyotaka na kile alichomiliki. Mungu anayo haki kulipa kisasi juuya maadui zake.

**nitalipa**
Ulipaji wa Mungu wa kisasi kunaongelewa kana kwamba ni kumlipa mtu ujira umfaao

**kuanguka katika mikono**
kupokea adhabu ya Mungu kunaongelewa kana kwamba mtu anaangukia katika mikono ya Mungu. Mikono" hapa inamaanisha uwezo wa Mungu wa kuhukumu.

## Hebrews 10:32

**siku zilizopita**
"wakati uliopita"

**baada ya kutiwa nuru**
kujifunza kweli kunaongelewa kana kwamba Mungu aliwasha taa juu ya mtu. AT: "baada ya kujifunza ukweli kuhusu Kristo"

**jinsi mlivyo vumilia mapingamizi makubwa**
"ni jinsi gani umevumilia mateso mengi"

**mlikuwa mmewekwa wazi katika dhihaka ya matukano na mateso**
"Watu waliwadhihaki kwa matukano na mateso ya wazi wazi"

**mlikuwa mmewekwa wazi katika dhihaka na matukano**
watu waliwaasi ninyi na kukutukana wazi

**mlikuwa mkishirkiana**
"mlijiuna na wale"

**urithi urio bora na wa milele**
Baraka za Munguza milele zinaongelewa kana kwamba ni mali

## Hebrews 10:35

**Maelezo ya Jumla:**
katika 10:37 ni nukuu kutoka kwa nabii Isaya katika Agano la Kale.

**Msiutupe ujasiri wenu, ulio na zawadi kuu.**
"Kukataa ahadi kunaongelewa kana kwamba ilikuwa ni kutupa kitu kisicho na thamani au kisicho na maana.

**kwa kitambo kidogo**
" kama Mungu alivyosema katika maandiko, kwa kila kitambo kidogo"

**kwa muda kitambo sana**
"mapema mno"

### Hebrews 10:38

**Maelezo ya Jumla:**
katika 10:38 mwandishi ananukuu kutoka kwa nabii Habakuki, ambayo moja kwa moja inafuata nukuu kutoka kwa nabii Isaya 10:37.

**mwenye haki wangu...kama akigeuka... pamoja naye**
Haya maneno yanamaanisha kwa watu wa Mungu wowote.AT: "watu wangu waaminifu ...kama mmoja wao akigeuka...kwa mtu huyo" au " watu wangu waaminifu... kama wakigeuka ... nao"

**kama akigeuka**
kukosa ujasiri na imani kunaongelewa kana kwamba ilikuwa nikugeuka kutoka kufuata njia.

**wanaogeuka kuelekea uangamivu**
kukosa ujasiri na imani kunaongelewa kana kwamba ilikuwa ni kugeuka kutoka katika kufuata njia.

**kwa kuzilinda imani roho zetu**
kuishi milele na Mungu kunaongelewa kana kwamba ilikuwa ni kutunza roho ya mtu, Na roho hapa inamaanisha mtu mzima mzima.

---



generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Chapter 11

1 Sasa imani ni hakika aliyo nayo mtu wakati atarajiapo kitu fulani kwa ujasiri. Ni hakika ya kitu ambacho
bado hakijaonekana. 2 Kwa sababu hii mababu zetu walithibitika kwa imani yao. 3 Kwa imani tunafahamu
kwamba ulimwengu uliumbwa kwa amri ya Mungu, ili kwamba kile kinachoonekana hakikutengenezwa
kutokana na vitu ambavyo vilikuwa vinaonekana. 4 Ilikuwa kwa sababu ya imani kwamba Habili alimtolea
Mungu sadaka ya kufaa kuliko alivyofanya Kaini. Ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba alisifiwa kuwa
mwenye haki. Mungu alimsifu kwa sababu ya zawadi alizoleta. Kwa sababu hiyo, Habili bado ananena,
ingawa amekufa. 5 Ilikuwa kwa imani kwamba Enoko alichukuliwa juu na hakuona mauti. "Hakuonekana,
kwa sababu Mungu alimchukua" kwa vile ilinenwa juu yake kuwa alimpendeza Mungu kabla ya
kuchukuliwa juu. 6 Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa kuwa ajaye kwa Mungu lazima
aamini kwamba Mungu anaishi na kwamba huwapatia zawadi wale wamtafutao. 7 Ilikuwa ni kwa imani
kwamba Nuhu, akiwa ameonywa na Mungu kuhusiana na mambo ambayo hayakuwa yameonekana, kwa
heshima ya ki Mungu alitengeneza safina kwa ajili ya kuiokoa familia yake. Kwa kufanya hivi, aliuhukumu
ulimwengu na akawa mrithi wa haki ambayo huja kupitia imani. 8 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Ibrahimu,
alipoitwa alitii na kwenda mahali ambapo alipaswa kupokea kama urithi. Alitoka bila kujua mahali gani
alikuwa anakwenda. 9 Ilikuwa ni kwa imani kwamba aliishi katika nchi ya ahadi kama mgeni. Aliishi
katika mahema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi wenzake wa ahadi ile ile. 10 Hii ni kwa sababu
alitarajia kuupata mji ambao mwenye kuubuni na mjenzi wake angelikuwa ni Mungu. 11 Ilikuwa ni kwa
imani kwamba Ibrahimu, na Sara mwenyewe, walipokea nguvu ya kutunga mimba ingawa walikuwa
wazee sana, kwa kuwa walimuona Mungu kuwa mwaminifu, ambaye aliwaahidia mtoto wa kiume. 12 Kwa
hiyo pia kutoka kwa mtu huyu mmoja ambaye alikuwa amekaribia kufa wakazaliwa watoto wasiohesabika.
Walikuwa wengi kama nyota za angani na wengi kama mbegu za mchanga katika ufukwe wa bahari. 13
Hawa wote walikufa katika imani pasipo kupokea ahadi. Isipokuwa, wakiwa wameziona na kuzikaribisha
kwa mbali, walikiri kwamba walikuwa wageni na wapitaji juu ya nchi. 14 Kwa wale wasemao mambo
kama haya wanaweka bayana kuwa wanatafuta nchi yao wenyewe. 15 Kwa kweli, kama wangekuwa
wakiifikiria nchi ambayo kwayo walitoka, wangelikuwa na nafasi ya kurejea. 16 Lakini kama ilivyo,
wanatamani nchi iliyo bora, ambayo, ni ya kimbingu. Kwa hiyo Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wao, kwa
kuwa ametayarisha mji kwa ajili yao. 17 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Ibrahimu baada ya kujaribiwa,
alimtoa Isaka. Ndiyo, yeye ambaye alipokea kwa furaha ahadi, alimtoa mwanawe wa pekee, 18 ambaye
juu yake ilinenwa, "Kutoka kwa Isaka uzao wako utaitwa." 19 IbrahImU alijua kwamba Mungu alikuwa na
uwezo wa kumfufua Isaka kutoka katika wafu, na kwa kuzungumza kwa lugha ya maumbo, alimpokea. 20
Ilikuwa ni kwa imani kwamba Isaka alimbariki Yakobo na Esau kuhusu mambo yajayo. 21 Ilikuwa ni kwa
imani kwamba Yakobo alipokuwa katika hali ya kufa, alimbariki kila mmoja wa watoto wa Yusufu. Yakobo
akaabudu, akiegemea juu ya fimbo yake. 22 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Yusufu wakati wake wa mwisho
ulipokaribia, alinena juu ya kutoka kwa wana wa Israel Misri na akawaagiza kuchukua pamoja nao mifupa
yake. 23 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Musa, alipozaliwa, alifichwa kwa miezi mitatu na wazazi wake kwa
sababu walimuona kuwa ni mtoto mchanga aliyekuwa mzuri, na hawakutishwa na amri ya mfalme. 24
Ilikuwa ni kwa imani kwamba Musa, alipokuwa mtu mzima, alikataa kuitwa mtoto wa binti Farao. 25
Badala yake, alichagua kushiriki mateso pamoja na watu wa Mungu badala ya kufurahia anasa za dhambi
kwa kitambo. 26 Alifikiri aibu ya kumfuata Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri kwa kuwa
alikaza macho yake katika zawadi ya wakati wake ujao. 27 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Musa alitoka
Misri. Hakuhofia hasira ya Mfalme, kwa kuwa alivumilia kwa kutazama kwa asiyeonekana. 28 Ilikuwa ni
kwa imani kwamba aliishika pasaka na kunyunyiza damu, ili kwamba mharibu wa mzaliwa wa kwanza
asiweze kuwagusa wazaliwa wa kwanza wa kiume wa waisrael. 29 Ilikuwa ni kwa imani kwamba walipita
katika bahari ya shamu kama katika nchi kavu. Wakati wamisri walipojaribu kupita, walimezwa. 30
Ilikuwa ni kwa imani kwamba ukuta wa Yeriko ulianguka chini, baada ya kuuzunguka kwa siku saba. 31
Ilikuwa ni kwa imani kwamba Rahabu yule kahaba hakuangamia pamoja na wale ambao hawakuwa
watiifu, kwa sababu alikuwa amewapokea wapelelezi na kuwahifadhi salama. 32 Na niseme nini zaidi?
Maana muda hautoshi kusimulia ya Gideoni, Barak, Samsoni, Yeftha, Daudi, Samwel na za manabii, 33
ambao kupitia imani walizishinda falme, walitenda haki, na wakapokea ahadi. Walizuia vinywa vya simba,
34 walizima nguvu za moto, walikwepa ncha ya upanga, waliponywa kutoka katika magonjwa, walikuwa
mashujaa vitani, na walisababisha majeshi wageni kukimbia. 35 Wanawake walipokea wafu wao kwa njia
ya ufufuo. Wengine waliteswa, bila kukubali kuachwa huru ili kwamba waweze kupata uzoefu wa ufufuo
ulio bora zaidi. 36 Wengine waliteswa kwa dhihaka na kwa vichapo, naam, hata kwa vifungo na kwa
kutiwa gerezani. 37 Walipondwa mawe. Walikatwa vipande kwa misumeno. Waliuawa kwa upanga.

Walikwenda kwa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi walikuwa wahitaji, wakiendelea katika maumivu na
wakitendewa mabaya
38 (ambayo ulimwengu haukustahili kuwa nao), wakitangatanga nyikani, milimani,
katika mapango na katika mashimo ya ardhini.
39 Ingawa watu wote hawa walikubaliwa na Mungu kwa
sababu ya imani yao, hawakupokea alichoahidi.
40 Mungu alitangulia kutupatia kitu kilichobora, ili
kwamba bila sisi wasingeweza kukamilishwa.

---

## Waebrania 11 Maelezo kwa jumla

### Muundo

Mwandishi anaanza sura hii kwa kuelezea nini maana ya imani. Baadaye anapeana mifano mingi ya watu waliokuwa na imani na jinsi walivyoishi.

### Dhana muhimu katika sura hii.

### Imani

Katika maagano yote mapya na ya zamani, Mungu alihitaji imani. Watu wengine wa imani walifanya miujiza na walikuwa wenye nguvu sana. Watu wengine wa imani waliteseka sana.

---

### Hebrews 11:1

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anaongea vitu vtatu kuhusu imani katika maelekezo haya mafupi.

**Sasa**
Neno hili limetumika hapa kufanya kupumzika katika fundisho lake kuu. Hapa mwandishi anaanza kufafanua maana ya "imani."

**Kwa hakika aliyo nayo mtu wakati atarajiapo**
"imani ni msingi alionao mtu katika tegemeo"

**hakika anatarajia**
Hapa jambo hili hurejea katika ahadi za Mungu, hususani uhakika walionao waamini wote wa Yesu kuwa kunawakati watakuwa na Mungu mbinguni milele.

**ambayo bado hayajaonekana**
"yale ambayohatujayaona" au "ambayo hayajaonekana"

**kwa sababu hii**
"Kwa sababu kulikuwa na matukio ya hakika ambayo yalikuwa hayajatokea"

**mababu walithibitishwa kwa imani yao**
"Mungu aliwathibisha mababu zetu kwa sababu ya imani yao"

**ulimwengu uliumbwa kwa amri ya Mungu**
"Mungu aliimba dunia kwa kuiamuru iwepo"

**kinachoonekana hakikuumbwa kwa vitu vinavyoonekana**
"Mungu hakuumba tunavyoviona kutokana na vitu vinavyoonekana"

### Hebrews 11:4

**Sentensi Unganishi:**
kisha mwandishi anatoa mifano mara nyingi kutoka Agano la Kale ya watu walioishi ka imani ingawa hawakupokea kile ambacho alikuwa amekiahidi wakati walipoishi duniani.

**alishuhudiwa kuwa mwenye haki**
'Mungu alishuhudia kwamba Habili alikuwa mwenye haki"

**Abel bado anazungumza.**
Yale aliyofanya Abel yanaendelea kutufundisha

**alishuhudiwa kuwa mwenye haki**
Mungu alimshuhudia kuwa mwenye haki"

### Hebrews 11:5

**Kwa imani Enoko alichukuliwa juu na hakuonja mauti**
Kwa imani Enoko hakufa kwa sababu Mungu alimchukua.

**Tazama Kifo**
Kufa.

**Kabla hajachukuliwa juu**
"Kabla Mungu hajamchukua juu"

**alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu. Maana dhaaniwa: 1) "Mungu alisema Enoki alikuwa amempendeza," 2) "Watu walisema Henoko alikuwa amempendeza Mungu."**
sasa pasipo imani

**Sasa hapa haimaanishi kwamba wakati huu lakini imetumika kuvuta usikivu kwa ajili ya kipengele kinachofuata.**
Pasipo imani haiwezekani kumpendeza yeye

**"mtu anaweza kumpendeza Mungu kama tu ana imani katika Mungu"**
yeyote ajaye kwa Mungu

**yeyote ajaye kwa Mungu**
anayetaka kumwabudu Mungu na kuwa sehemu ya watu wake kunaongelewa kana kwamba ni kuja kwa Mungu. "mtu yeyote anayehitaji kuwa sehemu ya Mungu"

**huwapatia zawadi**
"huwapatia wale"

**wale wote wamtafutao**
Kujifunza kuhusu Mungu na kufanya juhudi kumtii kunaongelewa kana kwamba mtu anamtafuta mtu mwingine.

### Hebrews 11:7

**baad ya kupewa ujumbe wa kiungu**
"Kwa sababu Mungu alimwambia yeye"

**kuhusu vitu ambavyo havijaonekana**
"kuhusu vitu ambavyo hapana hakuna hata mmoja amewahi kuviona kabla" au " kuhusu matukio ambayo hayajatokea bado"

**Ulimwengu**
Watu wanaoishi duniani wakati huo

**akawa mrithi wa haki**
Nuhu anaongelewa kana kwamba alikuwa akirithi mali ana utajiri kutoka kwa mwana familia. "alipokea kutoka kwa Mungu mwenye haki"

**hivyo kulinganga na imani**
"kwamba Mungu huwapa wale walio na imani katika yeye"

### Hebrews 11:8

**Alipoitwa**
"pindi Mungu alipomwita"

**alienda kwenye sehemu nje**
"Aliacha nyummba yake kwenda kwenye sehemu"

**Nchi ya ahadi**
"Nchi ambayo Mungu alimuahidia.

**aliishi katika nchi ya ahadi kama mgeni**
"aliishi kama mgeni katika nchi ambayo Mungu alikuwa amemuahidi."

**Warithi wenza**
"warith pamoja." Hii inaongea kuhusu Abrahamu, Isaka, na Yakobo kana kwamba walikuwa warithi ambao wangepokea urithi kutoka kwa baba yao.

**Mji ulio na misingi**
Mungu anaongelewa kana kwamba ni mbunifu na mjenzi.

**Mtaalam wa ujenzi**
Mtu ambaye anaunda majengo.

**mbunifu wa ujenzi**
mtu anayebuni majengo

### Hebrews 11:11

**Uwezo wa kushika mimba**
"Uwezo wa kuwa baba"

**walimwona Mungu kuwa mwaminifu, ambaye aliwapa ahadi**
"walimwamini Mungu, ambaye alikuwa amewaahidi vitu kuwa mwaninifu"

**alikuwa karibia na kufa**
"mzee sana kupata" au "mzee sana"

**Wazao wasioweza kuhesabika... wengi kama nyota angani na mbegu za mchanga zisizohesabika kwenye ufukwe ambao hauhesabiki**
Hii ilimuhusu Abrahamu kuwa na wana uzao mwingi sana.

**ambayo haihesabiki**
"ambayo mengi sana kuhesabu"

### Hebrews 11:13

**pasipo kupokea ahadi**
"pasipo kupokea ahadiambazo Mungu alikuwa ameawaahidi

**baada ya kuona na kuwasalimu kutoka mbali**
"baada ya kujifunza kile Mungu atakachofanya wakati ujao"

**walikiri**
walitambua" au walipokea"

**Walikuwa wageni na wapitaji katika nchi**
"wageni" na "wapitaji" kimsingi yanamaanisha kitu kimoja. Hii inasisitiza kwamba nchi haikuwa nyumbani kwao kweli. Walikuwa wakisubiri kwa ajili ya nyumbani kwao kweli ambapo Mungu ametengeneza kwa ajili yao.

**Nchi ya nyumbani.**
"Nchi ambayo wanatokea"

### Hebrews 11:15

**wa mbinguni**
"nchi ya kimbingu" au "nchi mbinguni"

**Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wao.**
"Mungu anafurahi kuitwa Mungu wao" au "Mungu anajivuna kuwa Mungu wao"

## Hebrews 11:17

**alipojaribiwa**
"pindi Mungu alipomjaribu"

**kwake ambaye ilikuwa imesemwa**
"kwake ambaye Mungu alisema"

**Kutoka kwa Isaka uzao wako utaitwa**
"Ni katika uzao wa Isaka amabao Mungu atafikiri uzao wako.

**kuongea kwa mafumbo**
namna ya kuongea." Hii ina maana kwamba mwandishi anachosema kisichukuliwe kama tukio ambalo linatokea kimwili. Mungu hakumleta Isaka kutoka kwa wafu.Lakini Abrahamu alikuwa anataka kumdhabihu Isaka wakati Mungu alipomzuia, ilikuwa kana kwamba Mungu alikmrudisha kutoka kwa wafu.

**Alimpokea tena**
"Abraham alimpokea Isaka tena

**ilikuwa kutoka kwao**
"ilikuwa kutoka kwa wafu

**alimpokea**
"Abrahamu alimpokea Isaka"

## Hebrews 11:20

**Yakobo aliabudu**
"Yakobo alimwabudu Mungu"

**Mwisho ulipokuwa umekaribia**
"alipokuwa amekaribia kufa"

**aliongeakuondoka kwa wana wa Israeli wangetoka Misri"**
"aliongea wakati wana wa Israeli wangeondoka Misri"

**wana wa Israeli**
"wana wa Israeli" au " uzao wa Israeli"

**aliwaelekeza kuhusu mifupa yake**
Yusufu alikufa akiwa Misri. Aliwataka waru wake kuchukua mifupa yake wakati wataondoka Misri ili kwamba waizike mifuka katika nchi ambayo Mungu alikuwa amewaahidi.

## Hebrews 11:23

**Musa, alipozaliwa, alifichwa na wazazi wake kwa miezi mitatu**
"Wazazi wa Musa walimfika kwa miezi mitatu baada ya kuzaliwa."

**alikua**
"Akawa mtu mzima

**alikataa kuitwa**
"aliwazuia watu kumuita"

**Dharau zitokanazo na kumfuata Kristo**
"udhoefu wa watu kutokumuheshimu kwa sababu alifanya kile ambacho Kristo angetaka"

**Elekeza macho yake katika zawadi ya mbele**
"Kufanya kile alichojua kuwa kitampatia zawadi huko mbinguni."

**kumfuata Kristo**
kumtii Kristo kunaongelewa kana kwamba walikuwa wakimfuata katika njia.

**kuweka mach yake katika zawadi yake**
Kufanya kile alichokifahamu kungemwezesha kupata taji mbinguni"

## Hebrews 11:27

**alivumilia kana kwamba alikuwa alimwona yeye asiye onekana**
Musa anaongelewa kana kwamba alimwona Mungu, ambaye haonekani.

**yule ambaye haonekani**
"yeye ambaye hakuna mtu anaweza kumwona"

**Kunyunyiza kwa damu**
Hii inamaanisha amri ya Mungu kwa Waisraeli kuchinja mwana kondoo na kusambaza juu ya kila muimo wa kila nyumba mahali ambapo waliishi Hii ingezuia muharibifu kutowaaribu wazaliwa wao wa kwanza.

**usiguse**
"usidhuru" au " usiue"

## Hebrews 11:29

**Maelezo ya Jumla:**
"wao" ya kwanza ina maanisha Waisraeli, na "wao" ya pili inamaanisha Wamisri na "wao" ya tatu inamaanisha kuta za Yeriko.

**Walipita**
Waisraeli walipita kupitia Bahari ya Shamu'

**Walimezwa**
"Maji yaliwameza Wamisri"

**walimezwa**
"Wamisri walizama ndani ya maji"

**Walikuwa wamezunguka kwa siku saba**
"Waisrael walitembea kwa kuzunguka kuta kwa siku saba"

**Aliwapokea wapelelezi na kuwahifadhi salama**
"Aliwaficha wapelelezi ili wawe salama

## Hebrews 11:32

**Sentensi Unganishi:**
mwandishi anaendelea kuongelea kwa kile ambacho Mungu angefanya kwa mababu wa Israeli.

**Niseme nini tena**
Mwandishi anatumia swali kusisitiza kwamba kuna mifani mingi ambayo aliyoinukuu.

**Muda hauta niruhusu**
"Sita kuwa na muda wa kutosha"

**Baraka**
Jina la mtu.

**ilikuwa ni kwa kupitia imani kwamba wali**
"ilikuwa ni kwa ajili ya imani wale wanaume kama hivi"

**walishinda**
"waliwashinda watu wa falme ngeni"

**Shinda**
Iliyoshinda

**Simamisha vinywa vya simba alizima nguvu ya moto... alikwepa makali ya ncha ya upanga**
Njia ambazo watu wa Israeli waliokoka kutoka kifo. "Simba hawakuwala... moto haukuwaunguza." Upanga haukuwaua."

**Waliponywa**
"walipokea uponyaji kutoka kwa Mungu"

**wakawa hodari katika vita, na wakashinda**
"wakawa hodari katika vita na wakashinda"

## Hebrews 11:35

**Wanawake walipokea wafu wao tena kwa ufufuo**
"Wanawake walipokea wafu waliokuwa wamekufa wakati Mungu alipowafufua"

**Wengine waliteswa... wengine waliumizwa na dhihaka na vipigo... walipondwa mawe ... walikatwa kwa msumeno... walichinjwa**
Wengine waliteseka wakati wengine wanadhihakiwa... na wakachapwa wengine walikufa kwa sababu ya kutupiwa mawe... wengine walikufa walipokatwa na misumeno... watu waliwaua

**ufufuo ulio bora**
Maana zinazo dhaaniwa 1) hawa watu watapata maisha bora mbinguni au 2)Watu hawa watapata ufufuo ulio bora zaidi ya wale wasio na imani.

**wenginne walijaribiwa katika kutukana na kuchapwa... wapondwa mawe. walikatwa kwa wawili. waliuawa kwa upanga**
watu waliwatukana na kuwapiga wengine... watu waliwaponda mawe.

**wengine walijaribiwa katika kutukanwa, na hata minyororo na vifungo**
Mungu aliwajaribu wengine kwa kuwaruhusu adui zao kuwa tukana na kuwachapa na hata kuwaweka vifungo"

**katika mavazi ya kondoo na mbuzi**
"wakiva tu ngozi za kondoo na mbuzi"

**hawakuwa na makao**
"hawakuwa na kitu" au " walikuwa masikini sana"

**Ulimwengu haikuwastahili**
"watu wa dunia hii haikuwastahili"

**mapango, na ndani ya mashimo ya ardhi**
"na wengine waliishi katika mapango na mashimo ya ardhi"

## Hebrews 11:39

**Ingawa watu hawa wote walikuwa wamehakikishwa na Mungukwa sababu ya imani yao, hawakupokea ahadi**
"Mungu aliheshimu hawa kwa sababuya imani yao, lakini wenyewe hawakupokea kile ambacho Mungu alikuwa amekiahidi"

**ahadi**
"kile ambacho Mungu alikuwa amewaahidi."

**ili kwamba pasipo yeye wasingeweza kukamilishwa**
" ili kwamba Mungu angetukamikamilisha sisi na wao pamoja"

## Chapter 12

1 Kwahiyo, kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashaidi, na tutupe kila kitu kinacho tulemea
pamoja na dhambi ambayo inatuzingira kwa urahisi. Tupige mbio kwa saburi katika mashindano
yaliyowekwa mbele yetu. 2 Tuyaelekeze macho yetu kwa Yesu, aliye mwanzilishi na mwenye kutimiliza
imani yetu, ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake alistahmili msalaba, akiidharau aibu yake,
na akakaa chini mkono wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu. 3 Maana mtafakarini yeye aliye stahimili
maneno ya chuki kutoka kwa wenye dhambi, dhidi yake mwenyewe ili kwamba msije mkachoka au
kuzimia mioyo yenu. 4 Hamjataabika au kuteseka mkishindana na dhambi kiasi cha kuishiwa damu. 5
Tena mmesahau kule kutiwa moyo ambako kunawaelekeza kama watoto wa kiume: "Mwanangu,
usiyachukuwe kwa wepesi marudia ya Bwana, wala usikate tamaa unapo rekebishwa na yeye." 6 Kwa
kuwa Bwana humrudi yeyote ambaye anampenda, na humwadhibu kila mwana ambaye humpokea. 7
Stahimili majaribu kama kurudiwa. Mungu hushughulika nanyi kama anavyoshughulika na watoto, maana
ni mtoto yupi ambaye baba yake hawezi kumrudi? 8 Lakini kama hakuna kurudiwa, ambako sisi sote
tunashiriki, basi ninyi ni haramu na si watoto wake. 9 Zaidi ya yote, tulikuwa na baba zetu kidunia wa
kuturudi, na tuliwaheshimu. Je haitupasi hata zaidi kumtii Baba wa kiroho na kuishi? 10 Kwa hakika baba
zetu walituadhibu kwa miaka michache kama ilivyoonekana sawa kwao, lakini Mungu hutuadhibu kwa
faida yetu ili tushiriki utakatifu wake. 11 Hakuna adhabu inayofurahisha kwa wakati huo. Huwa na
maumivu. Hata hivyo, baadaye huzaa tunda la amani ya utauwa kwa wale waliofundishwa nayo. 12 Kwa
hiyo inueni mikono yenu iliyolegea na kufanya magoti yenu yaliyo dhaifu kuwa yenye nguvu tena; 13
nyosheni mapito ya nyayo zenu, ili kwamba yeyote aliye mlemavu hataongozwa upotevuni lakini apate
kuponywa. 14 Tafuteni amani na watu wote, na pia utakatifu ambao bila huo hakuna atakayemwona
Bwana. 15 Muwe waangalifu ili kwamba asiwepo atakayetengwa mbali na neema ya Mungu, na kwamba
lisije shina la uchungu litakalochipuka na kusababisha shida na kukengeusha wengi. 16 Angalieni kuwa
hakuna zinaa au mtu asiye mtauwa kama vile Esau, ambaye kwa sababu ya mlo mmoja aliuza haki yake ya
kuzaliwa. 17 Kwa kuwa mnajua kwamba baadaye, alipotamani kurithi baraka, alikataliwa, kwa sababu
hakupata fursa ya kutubu pamoja na baba yake, hata ingawa alitafuta sana kwa machozi. 18 Kwa kuwa
hamkuja katika mlima ambao unaweza kuguswa, Mlima unaowaka moto, giza, kukatisha tamaa na
dhoruba. 19 Hamkuja kwa sauti za tarumbeta, au kwa maneno yatokanayo na sauti ambayo ilisababisha
kila wasikiao wasiombe neno lolote kusemwa kwao. 20 Kwa kuwa hawakuweza kuvumilia kile
kilichoamuliwa: "Ikiwa hata mnyama agusaye mlima, lazima apigwe kwa mawe." 21 Ya kutisha zaidi
aliyoyaona Musa alisema, "Nimeogopa sana kiasi cha kutetemeka". 22 Badala yake, mmekuja mlima
Sayuni na katika mji wa Mungu aliye hai, Yerualem ya mbinguni, na kwa malaika elfu kumi
wanaosherehekea. 23 Mmekuja katika kusanyiko la wazaliwa wa kwanza wote waliosajiliwa mbinguni,
kwa Mungu hakimu wa wote, na kwa roho za watakatifu ambao wamekamilishwa. 24 Mmekuja kwa Yesu
mpatanishi wa agano jipya, na kwa damu iliyonyunyizwa ambayo hunena mema zaidi kuliko damu ya
Habili. 25 Angalia kuwa usije ukamkataa mmoja ambaye anenaye. Kwa kuwa kama hawakuepuka
walipomkataa mmoja aliye waonya duniani, kwa hakika hatutaepuka ikiwa tutageuka mbali kutoka kwa
yule atuonyaye kutoka mbinguni. 26 Kwa wakati huo sauti yake ilitikisa dunia. Lakini sasa ameahidi na
kunena, "Bado mara nyingine tena sitatikisa dunia pekee, bali mbingu pia." 27 Maneno haya, "Mara moja
tena," inaonesha kutoweshwa kwa vitu vile vitetemeshwavyo, hivi ni, vitu vile ambavyo vimeumbwa, ili
kwamba vile vitu visivyotetemeshwa vibakie. 28 Kwa hiyo, tupokee ufalme ambao hautetemeshwi,
tufurahi katika hali ya kumwabudu Mungu kwa kukubali pamoja na kunyenyekea katika kicho, 29 kwa
maana Mungu wetu ni moto ulao.

---

## Waebrania 12 Maelezo kwa jumla

### Muundo na mpangilio

Baada ya kuwafundisha watu umuhimu wa adhabu, mwandishi anaanza mfuatano ya mahubiri. .

Watafsiri wengine wameweka kila msitari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 12:5-6, ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Nidhamu

Mungu anataka watu wake kutenda yaliyo mema.Wakifanya kile hakipendi, anatakikana kuwarekebisha ama kuwadhibu. Yeye hufanya hivi jinsi baba wa duniani huwarekebisha na kuwadhibu watoto wao wanaowapenda.

---

## Hebrews 12:1

**Sentensi Unganishi:**
Kwa sababu ya idadi kubwa ya waumini wa Agano la Kale, mwandishi anaongelea maisha ya imani ambayo waamini wanapswa kuishi na Yesu kama kielezo chao.

**Maelezo ya Jumla:**
inamaanisha mwandishi na wasomaji wake. Neno nyie linamaanisha wasomaji.

**Tumezungukwa na kundi kubwa la mashahidi**
" kundi kubwa la mashahidi linatuzunguka sisi" au "Kundi kubwa la mashahidi linasimama kama mfano kwetu."

**Mashahidi**
"Mashahidi" hapa inamaanisha waumini wa Agano la Kale katika sura ya 11 walioishi kabla ya shindano la imani ambayo waumini wanashindana sasa hivi.

**tuweke kando kila mzigo na unatuzonga kwa urahisi**
"mzito" hapana "dhambi inayozonga kwa urahisi" vinaongelewa kana kwamba mtu angeweza kuziondoa na kuzitua chini.

**Mwanzilishi na mkamilishaji**
"muumbaji na mkamilishaji." Hii inamaanisha kwamba Yesu ni chanzo imani ya waumini.Ndiye ambaye waumini wanamtumaini, na atahakikisha waumini wanafikia lengo lao.

**furaha iliyowekwa mbele yake**
Furaha ungetoka kwa Yesu kunaongelewa kana kwamba Mungu Baba aliyoiwekambele yake kufikia lengo.

**aliidharau aibu yake**
Hii inamaanisha hakujali kuhusu aibu ya ya kufa msalabani.

**alikaa mkono wa kuume**
"Mkono wa kuume" hapa unamaanisha sehemu ya heshima.

**kiti cha enzi**
"enzi" inamaanisha utawala wa Mungu kama mfalme.

**kuchoka katika mioyo**
"mioyo" inamaanisha mawazo ya mtu na hisia.

## Hebrews 12:4

**Hauateseka na dhambi vya kutosha kiasi cha kupoteza damu**
"Umeshindana na dhambi, lakini wengine wamefanya hivyo kiasi cha kupoteza damu

**dhambi, mdhambi, kutenda dhambi**
Neno "dhambi" linamaanisha matendo, mawazo, na maneno ambayo yako kinyume na mapenzi na sheria za Mungu. Dhambi pia inaweza kumaanisha kutokufanya kitu ambacho Mungu anahitaji sisi tufanye.

**damu**
Neno "damu" linamaanisha kimiminikka chekundu ambacho kinatoka kwa mtu katika ngozi ya mtu wakati anapoumia au kidonda. Damu huleta virubtubisho vya uzima katika mwili wa mtu. Damu pia inamaanisha uzima na inapomwagika inaonyesha kifo. watu walipotengeneza dhabihu, waliua mnyama na kumwaga damu yake juu ya madhabahu. Na hii iliwakilisha dhabihu ya uhai wa wanyama kulipa kwa ajili ya dhambi za watu.

**kutia moyo, utiaji moyo**
Maneno kutia moyo na utiaji moyo inamaanisha kusema na kufanya vitu vinavyosababisha mtu kupata faraja, tumaini, ujasiri na moyo.

**kulekeza, elekezo**
Neno "kuelekeza" na "elekezo" yanamaanisha kutoa maalekezo ya moja kwa moja kuhusu nini kifanyike.

**mwana, mwana wa**
Neno "mwana" linamaanisha mvulama au mwanaume katika uhusiano na wazazi wake.Inaweza pia kumaanisha uzao wa mtu mme au kwa mtu mwana aliye asiliwa.

**Bwana**
Neno "Bwana" linamaanisha kwa mtu ambaye anaumiliki au uwezo juu ya watu. Inapotumika kwa herufi kubwa ni cheo kinachomaanisha Mungu.

**huadhibu**
Neno "adhibu" linamaanisha kufundiisha watu kutii maelekezo au kanuni kwa tabia njema.

**upendo**
kumpenda mtu mwingine in kumjali mtu huyo na na kufanya vitu vitakavyo mnufaisha. Kuna maana tofauti za upendo katika baadhi ya lugha inaweza konyeshwa kwa kutumia maneno tofauti: 1 Upendo

utokao kwa Mungu kuna lengamazuri juu ya wengine hata kama kama haimnufaishi. Aina hii ya upendo unajali wengine bila kujali wanafanya nini. Mungu mwenyewe ni upendo na chanzo cha upendo wa kweli.

**adhibu, adhabu**
Neno adhibu maana ni kusababisha mtu kuteseka kwa sababu ya kukosea kwake.

### Hebrews 12:7

**Vumilia majaribu kama maonyo**
"Elewa nyakati wa mateso Mungu hutufundisha nidhamu"

**Mungu anashughulik na ninyi kama ashughulikavyo na wana**
Hii inalinganisha unidhamishaji kwa Mungu kwa watu wake kama baba anavyo wanidhamisha watoto.

**wana... mwana**
Hiii ina jumuisha wamaume na wanawake, AT: "watoto... mtoto"

**ni mtoto yupi ambaye baba yake hawezi kumrudi?**
Mwandishi anatumia swali kuelewesha kwamba ni kawaida kwa kila baba mzuri kuwarudi watoto wake.

**Lakini kama hakuna kurudiwa ambako sisi sote tunashiriki**
"Hivyo kama haujapata kurudiwa na Mungu kama anavyowarudi wana wake wote"

**basi ninyi ni haramu na sio wana wake**
wale ambao Mungu hawarudi kunaongelewa kana kwamba ni wana ambao wamezaliwa na mwanamke na mwanaume ambao hawajaoana.

### Hebrews 12:9

**baba katika mwili**
Neno "mwili" hapa linamaanisha mwanadamu.

**kama warudiaji/ wanaotunidhamisha**
wanao turudi

**Je hatupaswi hata zaidi kumtii Baba wa kiroho na kuishi?**
Mwandishi anatumia swali kusisitiza kwamba wangeweza kumtii Mungu Baba,

**na ishi**
"ili kwamba tuishi"

**Baba wa roho**
"Baba yetu wa kiroho" au Baba yetu wa mbinguni"

**ili tushiriki utakatifu wake**
"ili kwamba tuwe watakatifu kama Mungu alivyo mtakatifu"

**tunda la amani**
"Tunda" hapa ni alama na inaongelewa kana kwamba ni mtu aliye katika amani na ambaye alileta amani kwa wengine.

**tunda la utauwa**
Utauwa, ni hali ya mtu anaye mtii Mungu, inaongelewa kana kwamba ni tunda linakuwa juu ya mti. Mwandishi hapa anasema kwamba utauwa unaongezeka kama matokeo ya kurudiwa.

**wale waliofundishwa nayo**
"wale walio fundishwa kwa kurudiwa." Ambao Mungu amewafundisha kwa kuwarudi."

### Hebrews 12:12

**inueni mikono yenu iliyolegea na kufanya magoti yenu yaliyo dhaifu kuwa yenye nguvu. Nyosheni mapito ya nyayo zenu**
Katika namna hii mwandishi anaongea kuhusu kuishi kama wakristo na kuwasaidia wengine.

**njia iliyonyooka**
Kuishi kama kumuheshimu na kumtukuza Mungu kunaongelewa kana kwamba ni kufuata njia iliyonyooka.

**iliyo dhaifu haitapotoshwa**
katika mfano huu wa kukimbia mashindanoni, "dahaifu" inawakilisha mtu mwingine katika shindano aliyeumia na anataka kuandoka katika shindano.Hili "geuka" linawakilisha wakristo wenyewe.

**isipokuwa aponywe**
"badala yake aimalike" au "badala yake Mungu atamponya"

### Hebrews 12:14

**Maelezo ya Jumla:**
Esau, ambaye amesema katika maandishi ya Musa, inamaanisha kwa mwana wa kwanza wa Isaka na ndugu yake Yakobo.

**tafuteni kuwa na amani na kila mmoja**
" jaribu kuishi na kila mtu"

**na pia ambao bila huo utakatifu hakuna atakayemwona Bwana**
"na pia fanya bidii kuwa mtakatifu, kwa sababu ni watakatifu pekee ndio watakaomwona Mungu"

**pia utakatifu**
"pia tafuta utakatifu"

**atakaye tengwa/ pungukiwa na neema ya Mungu**
"hakuna mtu anapokea neema ya Mungu na kisha akaiachia" au " hakuna anaikataa neema baada ya kwanza kuamini katika yeye"

 generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

**kwamba hakuna shina la uchungu litakalo kua na kusababisha shida ili kwamba wengi wasichafuliwe kwalo**
kwamba hakuna yeyote anayekuwa kama mzizi mchungu, ambao unaweza kukua na kusababisha matatizo uharibifu kwa watu wengi"

**alikataliwa**
"baba yake, Isaka, alikataa kumbariki"

**kwa sababu hakupata fursa ya kutubu**
"kwa sababu haikuwa inawezekana kwa baba yake, Isaka, kubadilisha uamuzi wake"

**ingawa alitafuta sana kwa machozi**
Hapa aliyetafuta ni Esau

## Hebrews 12:18

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anakinzanisha katika waumini wakati wa Musa walipaswa kufanya chini ya sheria na kile ambacho waumini wa sasa wanapaswa kusihi baada ya kuja kwa Yesu chini ya agano jipya.

**Maelezo ya Jumla:**
Maneno haya "ninyi" "Nyie" inamaanisha waumini wa Kiebrania ambao mwandishi anawaandikia. Neno "wale" linamaanisha watu wa Israeli baada ya Musa kuwaongoza kutoka Misri. Nukuu ya kwanza inatoka katika maandishi ya Musa. Mungu anafunua katika ukurasa huu katika Waebrania kwamba Musa alisema alitetemeka alipoona mlima.

**kwa kuwa hamkuja katika mlima ambao unaweaz kuguswa**
kwa kuwa hamjafikia, kama watu wa Israeli walivyokuja, mlimani ambao unaweza kuguswa"

**ambao unaweza kuguswa**
Hii inamaanisha waumini katika Kristo hawajafikia mlima kama Mlima Sinai ambao mtu anaweza kugusa au kuona.

**hamjafikia sauti ya tarumbeta**
"Hamjafikia mahali ambapo palipo na mlio mkubwa wa tarumbeta"

**au kwa maneno yatokanayo na sauti ambayo ilisababisha kila waisikiayo wasiombe neno lolote kusemwa kwao**
"sauti" inamaanisha mtu anaye ongea. pale ambapo Mungu anaongea kwa namna ya kwamba wale waliosikia walimtaka asiongee neno jingine kwao"

**kilichoamliwa**
'kile ambacho Mungu aliamuru"

**lazima apigwe kwa mawe**
"ni lazima uiponde"

## Hebrews 12:22

**Maelezo ya Jumla:**
Abeli alikuwa mwana wa mwanamme na mwanamke wa kwanza, Adamu na Eva. Pia Kaini mwana wao alimuua Habili.

**Mlima Sayuni**
Mwandishi anaongea Mlima Sayuni, hekalu la mlima Yerusalem kana kwamba lenyewe ilikuwa mbingu, nyumbani kwa Mungu.

**Wamekuja**
Wamewasili

**Malaika elfu kumi**
"Idadi isiyohesabika ya malaika"

**mzaliwa wa kwanza**
Hii inaongea waumini katika Kristo kana kwamba ni wana ambao ni wazaliwa wa kwanza. Hii inasisitiza sehemu yao maalumu na faida kama watu wa Mungu.

**mmesajiliwa mbinguni**
"ambao majina yao yameandikwa mbinguni

**mpatanishi wa agano jipya**
Hii inamaana Yesu alisababisha agano jipya kuwepo kati ya Mungu na wanadamu

**Mmekamilishwa**
"ambao Mungu amewafanya wakamilifu"

**Damu ya kunyunyiza ambayo hunena zaidi kuliko damu ya Habili.**
"Damu ya Yesu iliyonyunyizwa ambayo inamaana kubwa zaidi kuliko damu ya Habili, ambaye aliuawa na Kaini"

**damu**
damu hapa inasimama kwa kifo cha Yesu, kama damu ya Habili inavyoisimama kwa kifo chake.

## Hebrews 12:25

**Sentensi Unganish:**
Baada ya kulinganisha uzoefu wa Waisraeli katika Mlima Sinai na uzoefu wa waumini baada ya Kristo kufa, mwandishi anawakumbusha waumini kwamba wana Mungu yuleyule anayewaonya leo. Hili ni onyo la tanzo kwa waumini.

**Maelezo ya Jumla:**
Hii nukuu inatoka kwa nabii Hagai katika Agano la Kale.

**usije ukamkataa anayeongea**
"msikilizeni anaye ongea.

**kama hawakuepuka**
"kama watu wa Israeli hakuepuka hukumu"

**aliyewaonya duniani**
Pengine 1) Musa aliye waonya duniani." au) Mungu aliyewaonya katika Mlima Sinai"

**kama tukigeuka kutoka kwa yule anayetuonya**
Kutmtii Mungu kunaongelewa kana kwamba mtu alikuwa akigeuka na kutoka kwake. "kama tusipomtii yeye anayeonya"

**sauti yake iliitikisa ardhi**
"Mungu alipoongea mlio wa sauti yake ilisababisha ardhi kutikisika"

**ilitikiswa... tikisa**
tumia neno ambalo tetemeko la ardhi inafanya katika kuitetemesha adrhi.

## Hebrews 12:27

**Maelezo ya Jumla:**
Nukuu hii hapa kutoka kwa nabii Hagai inarudiwa kutoka mstari wa mwanzo.

**kutoweshwa kwa vitu vile viteteshwavyo**
'Mungu ataondoa vitu vyote vinavyotetemeshwa"

**tetemeshwa**
Tumia neno kwa tetemeko la ardhi linachofanya katika kutembea kwenye ardhi.

**vilivyokwisha kuumbwa**
"kwamba amekwisha umba."

**hivi vitu ambavyo haviwezi**
'vitu ambavyo havitetemeki"

**kupokea ufalme**
"kwa sababu tunapokea ufalme au " kwa "sababu Mungu anatufanya sisi kuwa wanafamilia wa ufalme wake"

**tufurahi**
"tumshukuru Mungu"

**kunyenyekea katika kicho**
"kunyenyekea" na "kicho" yana maanshabiliana maana na inasisitiza ukuu wa unyenyekevu kwa sababu ya Mungu"

**Mungu wetu ni moto ulao**
Mungu anaongelewa kana kwamba ni moto ambao unaweza kuchoma kitu chochote.


generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

## Chapter 13

1 Basi upendo wa ndugu na uendelee. 2 Msisahau kuwakaribisha wageni, maana kwa kufanya hivi, baadhi
wamewakaribisha malaika pasipo kujua. 3 Kumbuka wote waliomo gerezani, kana kwamba mulikuwa nao
kule pamoja nao, na kama miili yenu ilitendewa kama wao. 4 Basi ndoa na iheshimiwe na wote na basi
kitanda cha ndoa kifanywe kuwa safi, kwa maana Mungu atawahukumu waasherati na wazinzi. 5 Basi njia
zenu za maisha ziwe huru katika upendo wa pesa. Muwe wanoridhika na vitu mulivyonavyo, kwani Mungu
mwenyewe alisema, "Sitawaacha ninyi kamwe, wala kuwatelekeza ninyi." 6 Basi tulidhikeni ili tusema kwa
ujasiri, "Bawa ni msaidizi wangu; Sitaogopa. Mwanadamu aweza kunifanya nini?" 7 Wafikirieni wale walio
waongoza, wale waliongea neno la Mungu kwenu, na kumbukeni matokeo ya mienendo yao; igeni imani
zao. 8 Yesu Kristo ni yeye jana, leo, na ata milele. 9 Usije ukaongozwa na mafundisho mbalimbali ya kigeni
kwani ni vizuri kwamba moyo ujengwe kwa neema, na siyo kwa sheria kuhusu chakula hayo
hayatawasaidia wale wanaoishi kwa hayo. 10 Tunayo madhabau ambayo wale wanaotumika ndani ya
hekalu hawana haki ya kula. 11 Kwa kuwa damu za wanyama, zilizotolewa dhabihu kwa ajili ya dhambi,
ililetwa na kuhani mkuu ndani ya sehemu takatifu, lakini miili yao ilichomwa nje ya kambi. 12 Kwa hiyo
Yesu naye aliteseka nje ya lango la mji, hili kwamba kuweka wakfu watu kwa Mungu kupitia damu yake.
13 Na kwa hiyo twendeni kwake nje ya kambi, tukizibeba fadheha zake. 14 Kwani hatuna makao ya
kudumu katika mji huu. Badala yake tutafute mji ambao unakuja. 15 Kupitia Yesu mnapaswa mara kwa
mara kujitoa sadaka ya kumtukuza Mungu, kumsifu kwamba tunda la midomo yetu likili jina lake. 16 Na
usisahau kufanya mazuri na kusadiana ninyi kwa ninyi, kwa kuwa ni kwa sadaka kama hiyo ndiyo Mungu
hupendezwa sana. 17 Tiini na kujishusha kwa viongozi wenu, kwani wanaendelea kuwalinda kwa ajili ya
nafsi zenu, kama wale watakaotoa hesabu. Tiini ili kwamba viongozi wenu waweze kuwatunza kwa
furaha, na sio kwa huzuni, ambayo haitawasaidia. 18 Tuombeni, kwani tuna uhakikwa kwamba tuna
dhamira njema, tunatamani kuishi maisha ya heshima katika mambo yote. 19 Na nyote ninawatia moyo
zaidi mfanye hivi, ili kwamba niweze kurudi kwenu hivi karibuni. 20 Sasa Mungu wa amani, ambaye
aliwaleta tena kutoka kwa wafu mchungaji mkuu wa kondoo, Bwana wetu Yesu, kwa damu ya agano la
milele, 21 Atawapa uwezo kwa kila jambo zuri kufanya mapenzi yake, akifanya kazi ndani yetu iliyo njema
ya kupendeza machoni pake, kupitia Yesu Kristo, kwake uwe utukufu milele na milele. Amina. 22 Sasa
ninakutia moyo, ndugu, kuchukualiana na neno la kutia moyo ambalo kwa ufupi nililiandika kwenu. 23
Fahamu kwamba ndugu yetu Timotheo ameshaachiwa huru, ambaye pamoja naye nitawaona kama
atakuja hivi karibuni. 24 Salimia viongozi wako wote na waumini wote. Wale wanaotoka Italia
wanakusalimia. 25 Na neema iwe nanyi nyote.

---

## Waebrania 13: Maelezo kwa jumla

### Muundo na mpangilio

Mwandishi anamalizia orodha ya mashauri aliyoyaanza katika sura ya 12. Halafu anawauliza wasomaji wake kumuombea anapomalizia barua hii.

Watafsiri wengine wametenga kila mistari wa ushairi kulia kuliko maandishi mengine ili isomeke kwa urahisi. ULB inafanya hivi na ushairi katika 13:6 ambayo ni maneno kutoka Agano la Kale.

### Dhana muhimu katika sura hii

### Ukarimu

Mungu anataka watu wake wakaribishe watu wengine kuja kwa nyumba zao kula chakula na hata kulala. Watu wake wanastahili wafanye hivi hata kama hafahamu vizuri watu wanaowaalika. Katika Agano la Kale, Abrahamu na binamu yake Lutu walionyesha ukarimu kwa watu ambao hawakuwafahamu. Abrahamu aliandaa chakula cha bei na Lutu akawakaribisha kulala kwake.Walikuja kufahamu baadaye kwamba watu hao walikua malaika.

---


generated on Thu Aug 24 15:41:29 2023

### Hebrews 13:1

**Sentensi Unganishi:**
katika kufunga sehemu hii, mwandishi anatoa maelekezo ya moja kwa moja kwa waumini namna wanapaswa kuishi.

**Basi na upendo wa kindugu uendelee**
"Endeleeni kuonyesha upendo wenu kwa waumini wengine kama mfanyavyo kwa mwana familia"

**Usisahau**
"hakikisha unakumbuka"

**wakaribisheni wageni**
"kuwaribisha wageni na kuwaonyesha wema"

### Hebrews 13:3

**kana kwamba mlikuwa mmefungwa pamoja**
"kana kwamba mlikuwa gerezani pamoja nao"

**Ndoa na iheshimiwe na watu wote na kila mmoja**
"wanaume na wanawake walio na kuolewa waliolewa ni lazima waheshimiane.

**kama miili yao ilitendewa kama wao**
Hii inawatia moyo waumini kufikiri kuhusu mateso ya watu wengine kama ambaavyo wangeweza kufikiri juu ya mateso yao.

**kitanda cha ndoa kiwe safi**
Hii inamaanisha tendo la ndoa kana kwamba n kitanda cha watu walioana. AT: "wanaume na wanawakewaheshimu mahusiano ya ndoa yao na sio kwenda na watu wengine"

### Hebrews 13:5

**tabia zenu ziwe huru lakini sio katika kupenda fedha**
"Msipende pesa"

**Mtosheke**
"Toshekeni"

**Bwana ni msaidizi wangu...kunifanya mimi**
Hii nukuu inatoka katika Zaburi ndani ya Agano la Kale.

**Sitaogopa. Mwanadamu atanifanya nini?**
Mwandishi anatumia swali kusisitiza kwamba haogopi watu kwa sababu Mungu anamsaidia.

### Hebrews 13:7

**tokeo la mwenendo wao**
"matoke ya

**kuiga imani yao**
Tumaini katika Mungu na njia ya uzima iliyoongozwa na viongozi hawa inaongelewa kama "imani ya kweli'

**ni yeye yule yule, leo, na milele**
"Jana" hapa ina maana muda wote uliopita.

### Hebrews 13:9

**Maelezo ya Jumla:**
Sehemu hii inamaanisha dhabihu ya wanyama walio wafanya waumini katika Mungu katika kipindi cha Agano Kale, ambayo inafunika dhambi zao kwa muda hadi kifo cha Yesu kilipokuja.

**msije mkabebwa na mafundisho mageni mbalimbali**
usisawichiwe kwa mafundisho mbalimbali kunaongelewa kana kwamba mtu alikuwa amechukuliwa kwa lazima.

**moyo unapaswa kuimarishwa**
"moyo" unasimama kwa ujasiri wa mtu, upendo, na ushupavu.

**ni vizuri kwamba moyo ujengwe kwa neema, na siyo kwa vyakula ambavyo haviwasaidii wale wanao tembea kwa hivyo**
"tunapata nguvu pale tunapofikilia jinsi Mungu ambavyo amekuwa mwema kwetu, lakini hatuwi na nguvu kwa kutii sheria za kuhusiana na chakula"

**vyakula**
Vyakula hapa vinasimama kuhusu sheria za chakula.

**wale wanaotembea kwa hizo**
Kuishi kunaongelewa kana kwamba ni kutembea.

**madhabahu**
madhabahu inasimama kwa sehemu ya ibada. Pia inasimama kwa ajili ya wanyama ambao makuhani katika dhabihu za agano la kale, ambavyo walichukua nyama kwa ajili yao na familia.

**damu za wanyama zilizotolewa dhabihu kwa ajili ya dhambi inaletwa na kuhani mkuu sehemu takatifu**
kuhani mkuu analeta ndani ya sehemu takatifu damu ya wanyama ambao makuhani waliwachinja kwa ajili ya dhambi.

**wakati miili yao inachomwa moto**
"wakati makuhani wanapochoma miili ya wanyama"

**nje ya kambi**
"mbali na mahali ambapo watu waliishi"

### Hebrews 13:12

**Sentensi Unganishi:**
Kuna ulinganifu kati ya dhabihu ya Yesu na dhabihu za hekalu ya Agano la Kale.

**Kwa hiyo**
" Kwa njia hiyohiyo" au "Kwa sababu miili ya kujitoa iliunguzwa nje ya kambi"

**nje yalango la mji**
"Nje ya mji."

**Kwa hiyo ngoja sasa twende**
Kumtii Yesu kunaongelewa kana kwamba ni mtu alipaswa kuacha kambi kwenda nje Yesu alipo.

**kubeba aibu yake**
kutokuwa na huruma kunaongelewa kana kwamba in chombo ambacho kinapaswa kubebwa katika mikono ya mtu au juu ya mgongo wa mtu.

## Hebrews 13:15

**dhabihu ya sifa**
Sifa inaongelewa kana kwamba ni dhabihu ya wanyama au uvumba.

**sifa ambayo ni tunda la midomo ambayo inakiri jina lake**
sifa inaongelewa kana kwamba ni tunda, na "midomo" inaongelewa kana kwamba ni miti inayozaa matunda. Kwa nyongeza "midomo" inawakilisha watu wakimsifu Mungu.

**Jina lake**
Jina la mtu linamwakilisha mtu.

**tusisahau kufanya mazuri na kusaidiana**
"mara zote tukumbuke kufanya mema na kusaidia wengine"

**na dhabihu hiyo**
Kufanya wema na kuwasaidia kunaongelewa kana kwamba ni dhabihu juu ya mimbari.

**zitunzeni nafsi/roho zenu**
roho za waumini,ambayo ni mwenendo wa maisha ya kiroho, yanaongelewa kana kwamba ni vyombo au wanyamaambao waangaliz wangeweza kutazama.

**sio kwa huzuni**
"huzunu" inasimama kama msiba au huzuni.

## Hebrews 13:18

**Sentensi Unganishi:**
Mwandishi anafunga kwa baraka na salaamu

**Tuombeeni**
"Tuombeeni"hapa anamanisha mwandishi na wenzake.

**tuna uhakika kwamba tuna dhamira njema/ safi**
njema/ safi hapa inamaanisha hatuna hatia.

**kwamba nitarudi tena kwenu hivi karibuni**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo tendaji. AT: "kwamba Mungu akipenda nitaondoa mambo yanayonizuia kuja kwenu"

## Hebrews 13:20

**Sasa**
Hii ni sehemu ya mpya ya barua. Mwandishi hapa anamsifu Mungu na anatoa maombi ya mwisho kwa wasomaji wake.

**mchungaji mkuu wa kondoo**
Kristo katika jukumu lake la kiongozi na mlinzi wa wale wanaoaminikatika yeye kunaongelewa kana kwamba ni mchungaji wa kondoo.

**kwa damu ya agano la milele**
"Damu" hapa linasimama kwa kifo cha Yesu, ambacho ni msing kwa agano ambalo litakalodumu milele kati ya Mungu na waumini katika Kristo.

**kuwakamilisha katika kufanya kila jambo jema ili kufanya mapenzi yake**
"kuwakamilisha" hapa inamaanisha kuwafanya "kuweza" au "kuwafundisha"

**afanye kazi ndani yetu**
Neno hili "yetu" inamaanisha kwa mwandishi na wasomaji wake.

**kwake uwe utukufu milele na milele**
ambaye watu wote watamsifu milele

## Hebrews 13:22

**Sasa**
Hii inaonyesha sehemu mpya ya barua. Hapa mwandishi anatoa maoni yake ya mwisho kwa wale anaowaandikia.

**ndugu**
Hii inamaanisha waumini wote anaowandikia wanume au wanawake.

**huchukuliana na neno la kutia moyo**
"kwa uvumilivu fikirini juu ya nilichokiandika kuwatieni moyo.

**neno la faraja**
"Neno" hapa linasimama kwa niaba ya ujumbe.

**amewekwa huru**
"hayuko tena gerezani"

## Hebrews 13:24

**wale wanaotoka Italia wawasalimu**
Maana zinazodhaaniwa ni 1) mwandishi hayuko Italia, lakini kuna kundi la waumini waliotoka Italia walio pamoja naye au 2) mwandishi yuo Italia anapoandika barua hii.

**Italia**
Hili ni jina la sehemu wakati huo. Rumi ilikuwa mji mkuu wa Italia.